# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581569

Jumapili Januari 28, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


**Mganga** kienyeji, mkewe wauawa kikatili usiku



UKURASA 4

**KESI KUZUIA IBADA**

DC aomba mahakamani ishtakiwe ofisi, siyo mtu binafsi

UKURASA 4

**Chanzo** ndoa nyingi kuishia njiani hiki hapa



UK. 11



**MWENDO WA BWANGA**

UKURASA 13

**UDUMAVU, UTAPIAMLO**

# Wakuu Mikoa sasa kitanzini

• **Rais** Samia atoa maelekezo mahususi kwao... *Ukurasa 2*




Rais Samia Suluhu Hassan, akikata keki kuadhimisha kumbukumbu ya siku yake ya kuzaliwa Januari 27.1960, baada ya kupanda mti katika eneo la Donge Muwanda, Zanzibar jana. Wengine ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman (kushoto), Sabrina Said Soud (wa pili kulia) na George Joshua kutoka Green Samia. **PICHA: IKULU**

## Mahakama yaagiza ndugu waingie katika usuluhishi mvutano mirathi

UKURASA 3

## Dk. Mwinyi afumua Baraza la Mawaziri, waziri aking'atuka



UK. 3


**MICHEZO** **YANGA: AZAM 'WABAYA WETU'** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

UDUMAVU, UTAPIAMLO

# Rais Samia aweka kitanzini Wakuu wa Mikoa

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameagiza wakuu wa mikoa na viongozi wengine wa serikali kutoa elimu kwa wananchi kuhusu lishe kwa watoto ili kumaliza tatizo la udumavu na utapiamlo.

Aliagiza hayo jana alipozungumza na wananchi wa Mkoa wa Njombe kwa njia ya simu wakati wa kilele cha Kampeni ya Lishe iliyofanyika Halmashauri ya Mji wa Njombe na kushirikisha wadau wa lishe, viongozi wa serikali na wananchi.

"Mimi nikushukuru sana Mkuu wa Mkoa kwa wazo hilo na niwashukuru viongozi wote wa mkoa wa chama na serikali kwa wazo hilo la kukutana na kutafakari suala la lishe.

"Niwaombe sana mwendeleze elimu kwa umma, umma ukituelewa, basi tatizo hilo litaondoka haraka," aliagiza Rais Samia.

Alisema kuwa ni aibu kwa Mkoa wa Njombe ambao unazalisha kila kitu, kuwa na udumavu mkubwa na utapiamlo mkubwa.

"Sasa mimi imani yangu kwamba mtalifanyia kazi na watoto wetu watakuwa vizuri. Ninataka kina Pindi (Waziri wa Katiba na Sheria) wengi watoke huko," alisema Rais Samia.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka alimweleza Rais Samia kwamba kampeni hiyo imefanyika kufuatia maelekezo yake aliyoyatoa mwaka jana kwa viongozi wa Mkoa wa Njombe kwenda kuchukulia jambo la lishe kama kipaumbele cha mkoa.

"Tumefanya kazi hiyo kwa kushirikiana na wadau wa afya wanaofanya kazi Mkoa wa Njombe - wenzetu wa UNICEF, lakini pia watu wa USAID kwenye mradi wao wa Lishe Mtambuka.

"Mheshimiwa Rais, UNICEF waliweza kuitikia maelekezo yako. Walikuja moja kwa moja kwetu kwamba wako tayari kufanya kazi na sisi, lakini pia chama mkoa kilipokea maelekezo yako na kuagiza viongozi wa serikali kuyatekeleza," alisema Mtaka.

Mkuu wa Mkoa alisema wamefanya kampeni ya lishe kwenye halmashauri sita za Mkoa wa Njombe na kukutana na watu zaidi ya 1,500 ikiwa ni sambamba na kliniki za kinamama wajawazito na kinamama wanaoonyonyesha.

"Tumeonana na makundi ya viongozi wa dini, viongozi wa vyama vya siasa wakiongozwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) lakini pia makundi ya mamalishe na babalishe.

"Tumefanya mikutano na makundi ya wajasiriamali, bodaboda kama vijana ambao pia ni wazazi watarajiwa na wanafunzi makundi yote ya shule za msingi na sekondari," alisema.

Mtaka aliongeza kuwa ametoa maelekezo shule zote za msingi na sekondari kuanzisha bustani za mboga, pia kutoa elimu kupitia taasisi za kidini sambamba na kukubaliana na baadhi ya halmashauri kuwa na miradi ya kuku kwenye shule kwa ajili ya kugawa mayai.

"Lakini pia tumekubaliana na wakurugenzi kwenye shule ambazo tutapata miradi, wale walimu ambao wamesoma michepuo ya kilimo na mifugo tuweze kuwahamishia kwenye shule hizo ili waunge mkono miradi hiyo na kufundisha watoto kwenye uhalisia," alisema Mtaka.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Njombe, Deo Sanga alisema wananchi wa Njombe wameipokea Kampeni ya Lishe kwa mwitikio mkubwa.

"Tumezunguka mkoa mzima tukiongozwa na mkuu wa mkoa na chama na leo (jana) tupo hapa kuhitimisha, lakini hili litakuwa ni suala endelevu na sisi tunakushukuru kwa miradi mbalimbali ambayo umekuwa ukitupatia, tunakushukuru sana," alisema Sanga.

Maadhimisho ya Kampeni ya Lishe Mkoa wa Njombe yenye kaulimbiu 'Kujza Tumbo si Lishe, Jali Unachomlisha', iliambatana na kumbukizi ya siku ya kuzaliwa kwa Rais Samia.




Rais Samia Suluhu Hassan akipanda mti wa muembe katika eneo la Donge Muwanda, Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

### UPANDAJI MITI

Katika kuadhimisha kumbukizi ya kuzaliwa kwa Rais Samia, miti zaidi ya 400 ilipandwa jana katika eneo la Donge Muwanda, Mkoa wa Kaskazini Unguja ili kurejesha hali ya asili ya mazingira ambayo yameathiriwa na uchimbaji wa mchanga. Hafla hiyo iliongozwa na Rais Samia.

Mkuu wa Nchi alisema mazingira, hasa visiwani Zanzibar yameathirika kwa kiwango kikubwa na kupelekea maji ya bahari kupanda katika makazi ya wananchi na kuathiri shughuli zingine za kijamii ikiwamo maeneo ya kilimo, hivyo ni vyema hali hiyo ikadhibitiwa mapema.

Alisema hali hiyo ni hatari na lazima kurejesha hali asilia kwa kupanda miti ili kudhibiti athari hizo za kimazingira zisidi kuleta hasara kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

"Katika siku hii tumeamua kupanda miti kwa sababu mazingira yetu ya Tanzania yameharibika, bahari inakuja juu kwa kasi. Kama visiwa tupo hatarini lakini hata maeneo ambayo si ya visiwa na wenyewe yanaliwa na bahari. Kwahiyo, tukipanda miti, tukirejesha mikoko hii hali itapunguza kasi yake," aliagiza.

Rais Samia alisema kupandwa miti hiyo kutapunguza kasi ya athari za kimazingira. Kama nchi ilikuwa izame ndani ya miaka 200 ijayo, sasa itakwenda miaka 500 ijayo, hivyo akataka wananchi kuendelea kupanda miti ili kuzuia mmong'onyoko.

Alitaka wananchi wanaoishi maeneo ya bahari wajitahidi kurejesha uoto wa mikoko katika fukwe ambapo miti hiyo husaidia maji ya bahari kutopanda juu katika makazi ya watu.

Rais Samia alisema upandaji miti ni biashara kubwa kwa sasa duniani na kuna biashara ya hewa ukaa. Unapokuwa na msitu mkubwa hulipwa kwa kutunza miti hiyo, hivyo ni vyema wananchi kupanda miti na kuitunza ili istawi na ikue na kuwa na msitu wa maana ambao utafaa kwa vizazi vijavyo.

Pia aliwataka viongozi wa mkoa huo kuzuia kuchimba mchanga holela hasa ikizingatiwa kuwa Zanzibar ni kisiwa na ina uhaba wa mchanga, lakini kuchimba mchanga holela ni kujichimbia shimo na kumezwa na bahari.

"Niwaombe sana wale wanaotoa vibali vya uchimbaji mchanga ikiwamo Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuangalia maeneo ya juu ndio yapewe vibali, lakini pia kusitisha uchimbaji wa matofali katika miamba," aliagiza.

Rais pia alielekeza miti iliyopandwa jana itunzwe ili istawi, hivyo wananchi lazima wawe walinzi wa miti hiyo na kuwataka wanafunzi wa kilimo kuruhusiwa kufanya utafiti katika eneo hilo.

Alisema Zanzibar ya miaka 50 iliyopita ni tofauti na ya sasa ambayo ilikuwa na haiba nzuri ya kimazingira.

Rais Samia ametimiza miaka 64 tangu kuzaliwa mwaka 1960 na katika hafla hiyo jana kulikuwa na ukataji keki ulionogesha shughuli hiyo.

Wananchi wa kijiji hicho cha Donge Muwanda walisema wamefarajika na upandaji miti katika eneo hilo ambalo sasa ni jangwa. Miti itarejesha haiba ya asili ya eneo hilo ambalo likuwa na uoto wake.

"Zoezi hili tumelipokea kwa furaha na bashasha tunaahidi kuwa miti hii tutaitunza na kuilinda ili ikue vizuri kwa faida yetu sisi vizazi vya sasa na vijavyo," alisema Juma Makame, mmoja wa wazee wa kijiji hicho.

### ZIARA YA MWANZA

Katika hatua nyingine, Rais Samia anatarajiwa kufanya ziara ya kikazi kwa siku mbili mkoani Mwanza inayotarajiwa kuanza kesho. Akiwa huko atakabidhi vifaa vya kisasa vya uvuvi kwa wavuvi zaidi ya 980 wa mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Vifaa hivyo hivyo ambavyo ni pamoja na boti za kisasa 55 na vizimba 222, vinatarajiwa kutolewa kwa wavuvi 989 kutoka mikoa ya Mwanza, Mara, Geita, Kagera na Simiyu katika shughuli itakayofanyika katika uwanja wa mpira wa miguu Nyamagana, jijini Mwanza.

Baadhi ya wavuvi na wakazi mkoani Mwanza, akiwamo Juma Issa, wametaja hatua hiyo ya kutolewa kwa boti za kisasa katika Ziwa Victoria itainua sekta hiyo na kusaidia kufanyika uvuvi wa kisasa sambamba na kuimarisha ufugaji samaki kwa njia ya vizimba kupitia vizimba vitakavyotolewa.

**-Imeandaliwa na Elizabeth John (NJOMBE), Rahma Suleiman (ZANZIBAR) na Vitus Audax (MWANZA)**


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**HENRI HYACINTHUS I.D VAN TIENEN** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T762EBR aina ya Toyota NOAH, Chassis No. SR500031159, Engine No. 3S7339559. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya Polisi:
**PHQ/PWA/MKU/619/2024**

**KUPOTEA KWA VYETI**



**LIU TOKEO SAIDI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. S0294/0051 Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MOUNT CARMEL GIRLS SECONDARY SCHOOL mwaka 2016.Cheti cha kuzaliwa pamoja na kitambulisho cha mpiga kura, vyeti hivi vimepotea mkoa wa Tanga. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Taarifa ya Polisi: TAN/TAN/RB/499902/2021.**

**IN THE DISTRICT CLURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**MISC CIVIL APPLICATION NO. 152 OF 2023**
**SIASA VICENT WILLIAM..........APPLICANT**
**VERSUS**
**ESTHER JULIUS KULWA........RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE OF MENTION**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention on 31 day of 01.2024 at 9:00am Before Hon. Mwaisaka – SRM.
You required to appear in this Court without Failure and you must produce to that day all the documents upon which you intended to reply in support of your case.
**GIVEN** under my hand and Seal of the Court this 24 day of 01.2024.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

## HABARI KITAIFA

MVUTANO WA MIRATHI

# Mahakama: Ndugu ingieni katika usuluhishi

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Mwanzo Nzega imeamuru familia inayovutana kusimamia mirathi ya Zena Shemshadini ambaye hakuacha watoto, mume, wazazi wala wajukuu, waingie kwenye usuluhishi kwa kuwa wanaovutana ni ndugu.

Mahakama imefikia uamuzi huo mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Abunas Sonyo baada ya kuibuka ndugu mwingine kuomba kusimamia mirathi hiyo wakati mahakama ilishamteua Karim Samji kusimamia.

Wakati mahakama hiyo inatoa uamuzi wa kumteua msimamizi wa mirathi, hakukuwa na pingamizi kutoka kwa wanafamilia. Baada ya uteuzi, aliibuka Salma Mohammed ambaye ni mtoto wa mdogo wa marehemu, akafungua shauri akiomba kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Baada ya mahakama kuona mvutano huo, iliamuru pande zote wafike kwenye usuluhishi Januari 31, mwaka huu.

Samji aliwasilisha kiapo mahakamani akidai marehemu ni mama yake mdogo. Alifariki dunia akiwa hana watoto, mume, wazazi wala wajukuu. Watoto ni dada zake na mwombaji ndiye mtoto pekee.

Alidai marehemu hakuacha wosia na maelezo hayo yaliungwa mkono na wajukuu, Gullam Siager na Haji Seager, hivyo mahakama ikamteua kusimamia mirathi hiyo.

Marehemu aliacha nyumba moja iliyoko Mtaa wa Ntinginya, wilayani Nzega. Usajili: NTC/NMSH/NTI/81.

Katika uamuzi wake, mahakama ilitoa amri kwamba msimamizi wa mirathi awasilishe mahakamani orodha ya mali za marehemu, alipe madeni aliyoacha marehemu kama yapo na apewe mirathi na awasilishe taarifa ya mirathi hiyo Januari 30, mwaka huu.

Wanafamilia katika mirathi hiyo ni wajukuu; Araf Seager, Azaz Seager, Haji Seager, Asha Seager, Gullam Seager, Fatuma Seager na Kasu Seager pamoja na Karim Samji ambaye ni mtoto.

Shauri lingine la mirathi lilifunguliwa na Salma Mohammed dhidi ya Karim mbele ya Hakimu Hilda Kibona akiomba apewe haki ya kusimamia mirathi hiyo.

Baada ya mahakama kuona mvutano huo, iliamuru ndugu wakae wazungumzie suala hilo wajue wanalimaliza vipi kama kwa kuafikiana ama la kwan sababu wote ni ndugu.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (wa tatu kulia) na Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma (wa pili kulia), wakiongoza maandamano ya uzinduzi wa Wiki ya Sheria Kitaifa, yaliyoanzia eneo la Mahakama Jumuishi na kuishia viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma jana. Wa (tatu kushoto) ni Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

WAZIRI KUJIUZULU...

# Dk. Mwinyi afumua Baraza la Mawaziri

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amefanya mabadiliko katika Baraza la Mawaziri, akiteua mrithi wa nafasi ya aliyekuwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Mohamed Said aliyejiuzulu wadhifa huo juzi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotiwa saini na Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Zena Ahmed Said, Rais Dk. Mwinyi amemteua Mudrik Ramadhan Soraga kuwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale.

Kabla ya uteuzi huo, Soraga alikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji, nafasi ambayo sasa iko wazi.

Rais Dk. Mwinyi pia amewabadilisha baadhi ya mawaziri na kuteua manaibu waziri wapya na mawaziri wawili kuwaweka pembeni katika baraza lake.

Waliowekwa pembeni ni Jamal Kassim Ali ambaye alikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Ikulu. Nafasi hiyo imechukuliwa na Ali Suleima Mrembo ambaye kabla ya uteuzi huo alikuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango. Mwingine aliyewekwa pembeni ni Masoud Suleiman Makame aliyekuwa Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi. Rais amemteua Shabani Ali Othman kuwa waziri katika nafasi hiyo. Kabla ya uteuzi huo, Othman alikuwa Naibu Waziri wa Maji, Nishati na Madini.

Rais Dk. Mwinyi pia amemteua Juma Makungu Juma kuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango. Kabla ya uteuzi huo, Makungu alikuwa Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Manaibu Waziri wapya walioteuliwa ni Salha Mohamed Mwinjuma (Ardhi na Maendeleo ya Makazi). Silha alikuwa Mwakilishi wa Viti Maalum Kundi la Vijana Mkoa wa Kusini Unguja.

Mwingine ni Zawadi Amour Nassor aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Maji, Nishati na Madini. Zawadi ni Mwakilishi wa Konde, Mkoa wa Kaskazini Pemba (CCM).

Rais Dk. Mwinyi amefanya uteuzi huo ikiwa ni siku moja baada ya kuridhia ombi la kujiuzulu kwa aliyekuwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale. Uteuzi mpya ulianza mara moja jana, kwa mujibu wa taarifa hiyo ya Ikulu.

## Wastaafu wapewa mbinu kukwepa kufilisika mafao

**Na Halfani Chusi**

WASTAAFU na wadau wengine wameshauriwa kutumia mifuko ya uwekezaji iliyoko chini ya Kampuni ya Uwekezaji (UTT AMIS) kwa lengo la kupata faida zaidi, kutunza na kuhifadhi fedha zao.

Ni ushauri uliotolewa jana jijini Dar es Salaam na Ofisa Masoko Mwandamizi wa mfuko huo, Rahim Mwanga wakati wa hafla iliyokutanisha waandishi wa habari na wahariri kwa lengo la kuwaeleza namna mifuko hiyo inavyofanya kazi.

Alitaja mifuko hiyo kuwa ni pamoja na ya Umoja, Watoto, Wekeza Maisha, Kujikimu na Ukwasi huku akisitiza kuwa ni muhimu kujiunga ili kutimiza malengo.

Alisema wastaafu wengi wakishapokea mafao yao, hufilisika ndani ya muda mfupi kutokana na kukosa njia nzuri ya uhifadhi wa fedha zao, hivyo kupitia UTT AMIS wanaweza kuweka fedha na ikajizalisha.

"Siyo wastaafu tu, bali pia hata wananchi wengine wanaruhusiwa kuwekeza fedha zao kwa lengo la kukuza mitaji na hatimaye wakatimiza malengo yao kama kujenga nyumba na shughuli zingine za kiuchumi," alisema Mwanga.

Alibainisha kuwa hadi sasa wana wawekezaji zaidi ya 300,000, akisisitiza kuwa mtu anapowekeza katika mifuko yao, anaweza kupata faida kadhaa ikiwamo kusomesha watoto kwa urahisi, kujenga nyumba, kununua viwanja na vitu vingine vyenye thamani kubwa.

"Tumekuwapo kwenye soko kwa muda mrefu, manufaa yako mengi ambayo wawekezaji wanapata. Tunaweza tukayaangalia katika nyanja mbalimbali; mfano tuna mfuko kwa ajili ya watoto, hivyo wazazi na walezi wanaweza wakautumia kwa ajili ya kuwawekea akiba na kuwekeza kwake kunaanzia Sh. 10,000 tu.

"Kuna watu wanahitaji kukuza mitaji kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi; kuanzisha biashara, kusomesha watoto, kununua viwanja na kujenga, vyote hivyo vinahitaji fedha na kuipata kwa mkupuo ni ngumu. Kwahiyo, wanaweza wakaanza kuwekeza kidogo kidogo wakakuza kipato chao kupitia mifuko yao," alisema.

Mwanga alisema mfano mzuri wanaoweza kunufaika na mifuko hiyo ni wastaafu, akiwa na ufafanuzi kuwa moja ya changamoto yao ni namna ya kutumia mafao. Hivyo, kupitia Mfuko wa Hati Fungani wanaweza wakawekeza huko na kupata gawiwo kila mwezi au kila baada miezi sita.

Pia alisema kuwa kupitia Mfuko wa Kujikimu wanaweza kupata gawiwo baada ya miezi mitatu au kwa mwaka mara moja.

Mwanga alishauri wananchi kuchangamkia fursa mbalimbali za mifuko yao kwa kuwa wengi wanafanya kazi ambazo hazina mafao.

# Mganga wa kienyeji, mkewe wauawa

**Na Shaban Njia**, KAHAMA

NGUSA Jiramba (58), mganga wa kienyeji na mkazi wa Kijiji cha Sungamile, Kata ya Mwalugulu, Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga, pamoja na mkewe Bugumba Mahola (52), wameuawa kwa kucharangwa mapanga na watu wasiojulikana usiku wa manane.

Chanzo cha mauaji hayo ya kikatili kinadaiwa kuwa ni wahalifu hao kuhitaji fedha zaidi ya Sh. 700,000 alizokuwa amezitunza mganga huyo kwa ajili ya kununua ng'ombe. Inadaiwa na wenyeji kwamba ilikuwa kawaida kwa mganga huyo kununua mifugo.

Akisimulia tukio hilo, Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Jumanne Ngomage alisema lilitokea Januari 20 mwaka huu saa saba usiku na zilisikika kelele za kuomba msaada wakati wakicharangwa mapanga huku wavamizi wakihitaji fedha.

Alisema watu hao walivunja mlango wa nyumba aliyokuwa anaishia mganga wa kienyeji na mkewe usiku wa manani na kuhitaji fedha.

Alidai kuwa kiasi kilichokuwapo wakati huo kwa mujibu wa sauti za marehemu, ni Sh. 700,000 lakini wavamizi walidai kiasi hicho hakiwezi kununua ng'ombe na baadaye sauti ya marehemu haikusikika tena.

Ngomage alisema kuwa baadaye ilisikika sauti ya mkewe ikitaja kiasi cha fedha hizo na kuomba asiuawe na baada ya muda mfupi sauti yake haikusikika tena na baada ya kufanya ukatili huo, wahalifu hao walikimbia kusikojulikana, lakini ufutiliaji ulibaini shoka lenye damu lilitupwa kwenye shamba la jirani na lilikuwa la familia ya mganga.

"Tukio la namna hii ni la pilli kutokea kijijini hapa. Awali lilitokea miaka mitatu iliyopita na aliyeuawa wakati huo alikuwa mganga wa kienyeji na mkewe wake na sasa limetokea tena ameuawa mganga wa kienyeji na mkewe, hivyo tunaomba serikali ifanye uchunguzi wake na kuwabaini wahusika ili lisiendelee kujitokeza tena," alisema.

Mtoto wa marehemu, Lukala Ngusa (26) mwenye ulemavu wa macho, alisema usiku wa tukio, alisikia kelele za wazazi wake wakiomba wasiuawe na kutaja kiasi cha fedha kilichokuwamo ndani, lakini baadaye hakusikia sauti zao tena na badala yake alisikia sauti za watu ambao hakuzifahamu, wakidai kuwa kiasi kilichotolewa hakiwezi kununua ng'ombe.

Alisema mzee wake alikuwa anafanya shughuli za uganga za kutibu watu mbalimbali na fedha alizokuwa anazipata alikuwa anaziwekeza kwenye ufugaji, alipendelea kununua ng'ombe. Alidai kuwa baadhi ya ndugu zake wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa hatua za upelelezi.

Mwanafamilia aliyekuwa analala nyumba moja na marehemu hao, Ester Juma (18) alisema kuwa usiku wa tukio hilo alifuatwa chumbani kwake na mmoja ya wavamizi ambaye alikuwa amevaa kofia ya kuficha sura akiwa na tochi kubwa, akamnyoshea panga lililokuwa na damu akimtaka alale na kwa uoga, alilala na hakupiga kelele.

Mwanafunzi wa kidato cha tatu wa Shule ya Sekondari Mwaluguli, Christina Ngussa alisema ameingiwa na hofu ya kumaliza masomo yake baada ya wazazi wake kuuawa na atashindwa kupata mahitaji yake ya shule, hivyo akaomba serikali kumsaidia ili kuhitimu masomo yake. Ana ndoto za kuwa mwanasheria.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi alithibitisha kutokea tukio hilo na kudai kuna baadhi ya wanafamilia wanashikiliwa na jeshi hilo na upelelezi unaendelea. Watakaobainika kuhusika na tukio hilo, watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

Kamanda Janeth aliwataka wananchi kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi tena kwa kufanya mauaji kwa kuwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume cha sheria na watakapobainika wote waliohusika na tukio, adhabu kali itachukuliwa dhidi yao ili iwe fundisho.



Mwenyekiti wa Mashindano ya Qur-aan, Shekhe Nurdeen Kishik akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu maandalizi ya mashindano ya Qur-aan ya 24 Afrika. Kushoto ni Katibu Mkuu wa Kamati ya mashindano Quraan wa Taasisi ya Alhikma, Salum Kiza. **PICHA: JUMANNE JUMA**

KESI KUZUIA IBADA

# DC ataka ishtakiwe ofisi, siyo mtu binafsi

**Na Zatifa Ramadhani,** SAUT

MKUU wa Wilaya ya Nyamagana, mkoani Mwanza, Amina Makilagi amewasilisha hoja mbili za pingamizi juu ya ombi lililowasilishwa na mleta maombi Januari 24, mwaka huu ambaye ni Mchungaji wa Kanisa la Assemblies of God Gospel Church International (AGGCI), Benson Kitonka kupitia wakili wake Gibson Ishengoma la kumtaka atekeleze amri ya Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza kuhusu shauri la madai ya ugomvi wa kanisa.

Hoja zilizowasilishwa na Mkuu huyo wa Wilaya kupitia Mwendesha Mashtaka Mwandamizi wa Serikali, Felishiani Mseti kumtaka mleta maombi kumshtaki Mkuu wa Wilaya kama cheo na si mtu (Amina Makilagi) kama ilivyowasilishwa mahakamani huko.

Mwendesha Mashtaka Mseti alidai kuwa mleta maombi anatakiwa kushtaki nafasi ya uamuzi ya Mkuu wa Wilaya na si mtu kwa kuwa anayeshtakiwa hafahamiki kisheria na inayofahamika ni ofisi inayompa nguvu ya kutoa uamuzi aliotoa katika mgogoro huo.

Alirejelea Sheria ya Kamishna wa Mkoa ya Mwaka 1997 kifungu cha kwanza na cha pili. Sheria inaelekeza kutakuwa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania. Atateuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika hoja ya pili, Mwendesha Mashtaka huyo alirejerea Sheria ya Usalama wa Taifa, kifungu cha 10 kinachomtambua Mkuu wa Wilaya kama Mwenyekiti wa Ulinzi wa Wilaya, hivyo akadai mletamaombi hana mamlaka ya kumshtaki kiongozi wa ulinzi na usalama. Alidai shauri hilo liondolewe mahakamani.

Wakili wa Mletamaombi, Gibson Ishemgoma alidai mapingamizi hayo yamepelekwa kimakosa mahakamani huko na kuhitaji yafanyiwe marekebisho kisheria kwa kuwa ushahidi ulikuwa tayari umekamilika.

Alidai kuwa hoja za mapingamizi ya mjibumaombi kwamba shauri hilo liondolewe mahakamani, hazikubaliki na wala si za kisheria.

Baada ya pande zote mbili kuwasilisha hoja zake, Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza, Wilbert Chuma, aliyekuwa anasikiliza shauri hilo la maombi madogo 68/2023, aliliahirisha mpaka Februari 5 mwaka huu itakapoitwa kwa ajili ya kutolewa uamuzi.

## PAC yataka OSHA itumike ununuzi samani serikalini

**Na Frank Monyo**

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeishauri serikali kutumia Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kuainisha viwango vya usalama na afya katika samani na vifaa mbalimbali vya ofisi kabla ya ununuzi kufanyika ili kuepuka kununua samani na vifaa visivyokidhi viwango stahiki.

Ni ushauri uliotolewa na kamati hiyo baada ya wajumbe wake kupatiwa mafunzo kuhusu masuala ya usalama na afya mahali pa kazi yaliyotolewa na wataalamu wa OSHA wakiongozwa na Mtendaji Mkuu, Khadija Mwenda.

Mwenyekiti wa PAC, Naghenjwa Kaboyoka, alisema kupitia semina hiyo, wamebaini samani na vifaa mbalimbali visivyozingatia viwango vya usalama na afya vimeendelea kununuliwa katika majengo na ofisi za serikali licha ya kuwapo taasisi ya OSHA ambayo ingeweza kutoa ushauri juu ya viwango stahiki.

Mwenyekiti huyo ameeleza kuwa OSHA inapaswa kushirikishwa kikamilifu katika miradi ya ujenzi wa majengo ya serikali hususan katika Mji wa Serikali unaoendelea kujengwa katika eneo la Mtumba jijini Dodoma ili ujenzi huo uzingatie kuwapo miundombinu rafiki kwa ajili ya kulinda afya na usalama wa watumishi wa umma na wananchi kwa ujumla.

"Tumeishauri taasisi yetu ya OSHA kwenda kwenye taasisi zote za serikali na mashirika ya umma kuwaeleza kuhusiana na umuhimu wa kununua samani na vifaa vinavyozingatia afya na usalama kwa wafanyakazi ili kuepuka hasara inayoweza kusababishwa na ununuzi wa samani na vifaa visivyokidhi viwango stahiki katika kulinda afya na usalama wa watumiaji wake.

"Imekuwa ni muhimu kwa kamati yetu kuwa na ufahamu wa masuala haya ya usalama na afya kwanza kama wawakilishi wa wananchi ambao tunawajibika kuwapa elimu wananchi wetu huko majimboni.

"Elimu tuliyoipata itatuwezesha kuishauri serikali kuhusiana na matumizi mazuri ya fedha za umma hususan katika kuimarisha afya na usalama wa wafanyakazi nchini," alisema.

Baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo walieleza umuhimu wa semina hiyo kwao.

"Tumepata fursa ya kupata wasilisho kuhusu kazi, sheria na miongozo ambayo OSHA wamekuwa wanatoa kwenye maeneo ya kazi, lakini nikiri kwamba kwa nchi kama yetu inayopambana kukuza uchumi wake, tunawahitaji sana OSHA ili watoe miongozo ya uzalishaji unaozingatia viwango vya usalama na afya, jambo ambalo litawezesha bidhaa zinazozalishwa kuwa katika ubora unaokubalika hata katika masoko ya kimataifa," alisema Anatropia Theonest, mjumbe wa PAC. Mjumbe Venant Protas aliipongeza OSHA kwa maboresho ambayo imeendelea kufanya katika utendaji wake.



Terry Strong (wa pili kushoto), akimtunuku cheti Julieth Lwehabura ambaye ni mmoja wa wanafunzi 50 wa vyuo vikuu walioshiriki katika programu ya mafunzo kwa vitendo kwa mwaka 2023, mjini Geita juzi. Wanaoshuhudia ni Meneja Mwandamizi Rasilimali Watu wa kampuni hiyo, Charles Masubi (kushoto) na Meneja wa Mafunzo na Maendeleo, Dominic Marandu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DPP ajivunia kupunguza mahabusu gerezani

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MKURUGENZI wa Mashtaka ( DPP), Sylvester Mwakitalu ametaja mafanikio yaliyopatikana kutokana na uendeshwaji haraka wa mashtaka ikiwamo kupungua mahabusu magerezani baada ya kupungua kwa mashauri ya muda mrefu mahakamani.

Mwakitalu alibainisha hayo juzi alipofungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka uliofanyika mkoani Mwanza, akisema kuwa awali kulikuwa na mrundikano wa kesi katika mahakama, lakini kwa sasa idadi imepungua kwa kiasi kikubwa.

Alisema hali hiyo inatokana na upelelezi kumalizika mapema na mashauri ya jinai kuendeshwa na kuamuliwa kwa muda mfupi ikiwa ni pamoja na kesi kusikilizwa kwa haraka na mfululizo katika mahakama husika. Alisema kesi za muda mrefu zimesikilizwa na kutolewa uamuzi. Kwa mujibu wa taarifa ya Magereza ya Desemba 2023, kuna mahabusu takribani 8,000 nchi nzima.

"Kulikuwa na kesi zimekaa miaka miwili lakini sasa inasikilizwa kwa haraka. Mashauri ya mauaji yanapelelezwa na kukamilisha upelelezi ndani ya siku 90 yanakuwa tayari kusikilizwa.

"Hiyo imetupa matokeo chanya hasa mahabusu wengi wa makosa ambayo hayana dhamana kesi zao zinasikilizwa haraka na kutolewa uamuzi kwa wakati," alisema Mwakitalu.

Kuhusu utaratibu wa makubaliano wa kukiri makosa, DPP alisema ulianza kutumika tangu mwaka 2019 na katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, hawakupokea malalamiko kuhusu mfumo huo wa kisheria baada ya kufanya marekebisho ya kimuundo katika kushughulikia kesi hizo.

Alisema utaratibu huo una faida nyingi ikiwamo kesi nyingi kumalizika kwa muda mfupi. Kesi ambayo ingechukua miaka miwili hadi mitatu ikisikilizwa na kuleta mashahidi, sasa inaweza kumalizika ndani ya siku mbili au tatu.

Alisema faida nyingine ni mtuhumiwa kutoa taarifa ambazo zitasaidia kupatikana mtandao wa uhalifu kwa kutoa taarifa za uhalifu mkubwa unaofanyika kwa makubaliano ya yeye kupunguziwa adhabu na hiyo imewapa faida kubwa kwa kuwa taarifa zao zimeweza kuwasaidia kukabiliana na uhalifu mkubwa.

"Ninapenda kutoa wito kwa wananchi kama kuna mwenye malalamiko kuhusu mfumo huu awasilishe malalamiko yake kwenye ofisi zetu," alisema Mwakitalu. Juma Katanga, Katibu wa Baraza la Wafanyakazi Ofisi ya DPP, alisema serikali inapaswa kuangalia namna ya kuiwezesha ofisi ya DPP kwa bajeti ili kuboresha maslahi ya watumishi kwa maslahi ya taifa kutokana na taasisi hiyo kuwa nyeti.

# RC: Marufuku viongozi kuzuia utekelezaji tuzo za mahakama

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Martin Shigela amepiga marufuku watendaji na viongozi kuzuia utekelezaji uamuzi wa mahakama katika hukumu zake.

Shigela alitoa agizo hilo wakati wa ufunguzi wa Wiki ya Sheria jana katika viwanja vya EPZ, Bombambili, Geita.

Alisema "sote kwa pamoja watendaji na viongozi wa ngazi zote wawe wa vitongoji, vijiji, kata, wilaya na mkoa lazima tuheshimu muhimili wa mahakama kwa sababu sote kwa pamoja ndiko tunapata haki zetu.

"Niwasihi sana sote kwa pamoja tujiepushe kuzuia utekelezaji hukumu ya mahakama kwa sababu kuzuia utekelezaji wa hukumu ya mahakama kunaweza kukupelekea wewe ukashtakiwa," alitoa hadhari.

Alisema wakiona mtu yeyote anazuia utekelezaji hukumu ya mahakama, wamkamate wampeleke mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake na kila mtu atekeleze amri za mahakama.

Mtekelezaji wa Tuzo za Mahakama Mkoa wa Geita, Ngwandu Tenga alisema changamoto iliyopo katika utekelezaji tuzo za mahakama ni pamoja baadhi ya wanasiasa kuzuia utekelezaji kwa maslahi yao binasfi, jambo ambalo linatia doa na ni uchonganishi wa mihimili.

Tenga alisema alisema wanasiasa kuingilia utekelezaji uamuzi wa mahakama kunasababisha kuchelewa utimizaji wa tuzo.

Pia aliwataka viongozi wazingatie miiko ya utumishi wa umma na utawala wa sheria ili wasiwe chanzo cha migogoro isiyoisha.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Tanzania Masjala Ndogo ya Geita, Kevin Mhina alisema amezipokea changamoto hizo zilizotolewa na Mtekelezaji wa Tuzo za Mahakama Mkoa wa Geita, Ngwandu Tenga na atazifanyia kazi.

# GGML yaaga wanafunzi 50 waliopata mafunzo kazini

**Na Halfani Chusi**

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imewaaga na kuwapatia vyeti wanafunzi 50 kutoka vyuo vikuu waliokuwa wanafanya kazi katika mgodi huo kama sehemu ya mafunzo kwa vitendo kupitia Mpango wa Mafunzo Kazini kwa mwaka 2023.

Wanafunzi hao ambao kati yao wa kike ni 30 na 20 wa kiume walipokewa Februari mwaka jana, waliagwa mwishoni mwa wiki iliyopita mkoani Geita.

Kati yao, 15 wamefanikiwa kubaki ndani ya kampuni hiyo; watano wamepatiwa mkataba wa kudumu na wengine 10 wamepatiwa mkataba wa muda chini ya taratibu za programu hiyo ya wahitimu.

Hatua hiyo ni mwendelezo wa mpango wa GGML wa kuchukua wanafunzi wa vyuo vikuu na kuwapatia uzoefu wa kufanya kazi katika fani mbalimbali ndani ya mgodi huo kwa lengo la kuunga mkono mipango ya serikali ya kuimarisha uwezo wa wahitimu ili kuajiriwa.

Akizungumza katika hafla ya kuaga wahitimu hao, Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Terry Strong alipongeza wanafunzi hao kwa kudumisha weledi na juhudi katika kazi walizokuwa wanazifanya kwa kipindi cha mwaka mmoja ndani ya mgodi huo.

Alisema wanafunzi hao walikuwa wanajituma kwa bidii na kuonesha uwezo wao katika nyanja mbalimbali walizokuwa wamepangiwa na wasimamizi wao ndani ya GGML.

Strong aliwaomba waende kuwa mabalozi wema katika kuitangaza GGML kwa yale mema yote waliyojifunza kipindi chote cha mwaka mzima.

Sambamba na hayo, Mkurugenzi Mtendaji huyo pia alisema GGML itachukua wanafunzi 40 katika mpango huo wa kuwapatia mafunzo kwa mwaka huu wa 2024. Kati yao 20 watakuwa wa kike na 20 wa kiume.

Wakizungumza baada ya kumaliza mafunzo hayo, wanafunzi hao, akiwamo Julieth Lwehabura, walishukuru GGML kwa kuwapokea na kuwapatia uzoefu wa kipekee ambao utakuwa chachu kwao katika kuendelea kupiga hatua katika taaluma zao.

Shamimu Mfinanga alisema uzoefu waliopata ndani ya GGML unakwenda kufungua milango ya fursa kwao, ikizingatiwa hiyo ni kampuni kubwa iliyojitolea kuwa mfano wa kuigwa kwa kuwajali wanafunzi wanaohitimu vyuo vikuu nchini.

Tangu kuanza kwa programu hiyo mwaka 2009, GGML imeshatoa mafunzo kwa wanafunzi 218 kutoka vyuo mbalimbali. Kati yao, wanawake ni 131 na wanaume ni 87.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maafa haya kila majira ya mvua yapatiwe ufumbuzi

**BAADHI** ya maeneo mkoani Dar es Salaam yaligeuka madimbwi na mabwawa ya maji kutokana na mvua inayoendelea kunyesha tangu kuanza kwa mwaka huu. Maeneo kama Boko, Kunduchi, Basihaya, bonde la Msimbazi, Tabata, Tegeta, Mbezi, Mikocheni, Kinondoni, Msasani na Magomeni, mvua hiyo ilisababisha matatizo yakiwamo vifo vya watu, nyumba kubomoka na watu kupoteza mali.

Mbali na Dar es Salaam, baadhi ya mikoa kama Morogoro, Mwanza, Shinyanga na Arusha ambako mvua kubwa ilinyesha, kulitokea pia madhara ikiwamo vifo, uharibifu wa miundombinu, kukatika mawasiliano kati ya mkoa na mkoa na maeneo kadhaa kukumbwa na magonjwa ya mlipuko hasa kipindupindu.

Kubwa zaidi, wakati mwaka 2023 unakaribia ukingoni, madhara makubwa yalitokea katika Mlima Hanang na kusababisha vifo na wananchi kukosa mali pa kuishi baada ya tope lililoandamana na maporomoko na mvua.

Pongezi ziende kwa serikali na wadau wengine kwa kutoa misaada ya kibinadamu kama vyakula, nguo na sehemu za muda kwa ajili ya kujisitiri.

Kwa ujumla, mvua hiyo iliyonyesha na inayoendelea kunyesha, ni dhahiri kwamba maafa zaidi yanaweza kujitokeza kutokana na hali halisi iliyoko katika maeneo mbalimbali ya nchi, iwapo hatua madhubuti hazitachukuliwa.

Kwa maneno mengine, matatizo hayo yanayotokea kila mvua inaponyesha, yamekuwa kama hadithi zisizo na mwisho.

Ni wakati mwafaka wa serikali kuweka mipango mahususi katika kuimarisha miundombinu ili maafa kama hayo yasijirudie katika maeneo mengi nchini na kuathiri nguvu kazi muhimu kwa maendeleo ya taifa pamoja na uharibifu wa mali.

Jambo la msingi la kufanya ni kuhakikisha miundombinu mipya injayojengwa inasaidia kuepusha majanga kwa jamii. Hiyo inatokana na malalamiko yanayoendelea katika Manispaa ya Morogoro kwamba katika kata kadhaa, kumekuwa na mafuriko yanayosababisha wananchi kukumbwa na majanga kutokana na ujenzi wa reli ya kisasa baada ya mkandarasi kutengeneza mfereji unaokwenda kwenye makazi ya watu, hivyo mvua inaponyesha maji hukimbilia huko.

Hakuna muujiza unaoweza kuondoa au kukwamu majanga yanayojitokeza kila mwaka wakati wa mvua isipokuwa serikali kwa kushirikiana na wadau, kuandaa mipango kabambe na endelevu ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kuepusha maafa hayo.


Mfano ni katika mkoa wa Dar es Salaam ambako baadhi ya maeneo hufurika maji na kusababisha baadhi ya njia kufungwa. Moja ya maeneo hayo ni Kinondoni kati ya Mkwajuni na Magomeni Morocco, ambapo mvua iliyonyesha hivi karibuni ilisababisha eneo hilo kufungwa kwa sababu ya bonde la Mkwajuni kujaa maji.

Kutokana na tatizo hilo, swali la msingi ambalo pengine limekosa majibu kwa muda mrefu ni nini kinachofanya pasitengenezwe mfereji mkubwa wa kupitisha maji kutoka Sinza hadi bonde la Mkwajuni na hatimaye maji hayo kwenda moja kwa moja baharini?

Hilo pia lina uhusiano na eneo la Jangwani ambalo limekuwa likikumbwa na maafa kama hayo kila mwaka mvua inaponyesha.

Ni vyema majibu kuhusu matatizo yanayojitokeza kila mwaka wakati wa mvua yakapatiwa ufumbuzi ili kunusuru maisha na mali za wananchi na wakati huo huo, kupunguza hasara zinazotokana na maafa hayo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Ruhusa maandamano ya CHADEMA, Rais ameupiga mwingi



Na Sabato Kasika

**TANGU** kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi zaidi ya miaka 30 iliyopita, kumekuwapo vikwazo kuruhusu maandamano ya amani ya vyama vya siasa katika awamu mbalimbali za uongozi wa nchi.

Vikwazo hivyo huambatana na sababu mbalimbali ambazo hutolewa kuzuia maandamano hayo, ikiwamo kuwapo uvunjifu wa amani na nyingine nyingi.

Lakini chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, maandamano amani yaliyoandaliwa na CHADEMA, yamefanyika kwa amani na kumalizika kwa amani.

Viongozi wa vyama vya upinzani vinasema ni haki yao kikatiba kuandamana ili kufikisha kwa serikali, umma na dunia ujumbe ambao vimekusudia ufike.

Kwa mfano, CHADEMA ilikuwa na hoja kadhaa ambazo imeona njia pekee ya kuzifikisha ni kufanya maandamano yaliyofanyika Januari 24 mwaka huu.

Baadhi ya hoja hizo ni kutaka serikali iondoe miswada mitatu ya sheria iliyowasilishwa bungeni ambayo ni Muswada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi, Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani na tatu Muswada wa Sheria ya Vyama vya Siasa.

Hoja nyingine ni kufanya marekebisho madogo ya katiba itakayoendana na mahitaji ya uchaguzi huru na haki.

Kupunguza gharama za maisha kwa kuondoa tozo kwenye bidhaa mbalimbali, kukomesha matumizi ya anasa kwa serikali na viongozi wa umma.

Pamoja na kwamba hoja hizo zinaigusa serikali, Rais Samia ameruhusu maandamano hayo ili chama hicho kiOnyeshe dunia kuwa chama tawala kimeshindwa kutimiza matarajio ya umma wa Watanzania.

Bila ukomavu wa kisiasa, ninadhani isingekuwa rahisi kuruhusu maandamano ambayo yanapinga serikali yake, kwa kuwa Rais amekomaa kisiasa, amekubali wafuasi wa chama hicho waandamane.

Hatua hiyo imeonyesha kuwa Rais yuko makini na hataki kuumiza watu wake anaowangoza, ndio maana wameandamana na kufikisha ujumbe wao kwa amani.

Kimsingi, ninadhani Rais anajua si vyema kuanza kupambana na upinzani wakati huu wa kuelekea kwenye uchaguzi wa mwaka huu na uchaguzi mkuu.

Ninaamini kwamba, CHADEMA wamefikisha ujumbe walioukusudia haya kama hautatiliwa maanani au vinginevyo, lakini kitendo cha kuruhusiwa kuandamana kinaonyesha umakini wa Rais katika uongozi.

Uamuzi wa kuruhusu maandamano badala ya mabomu ya machozi unaonyesha jinsi ambavyo Rais amedhamiria kuwaleta Watanzania pamoja bila kujali itikadi za vyama vyao.

Hatua hiyo ya kuruhusu maandamano, inaweza kuwa njia mojawapo ya kuondoa kero ambayo wapinzani walikuwa wakiilalamikia kwa muda mrefu ya kutoruhusu maandamano na kusababisha manung'uniko.

Ninadhani kwa hatua hiyo, hawana lawama tena kwa Rais kuhusu maandamano. Wameruhusiwa, wameandamana kama walivyotaka na sasa roho zao zimetulia baada ya 'kutema nyongo'.

Sina budi kumpa hongera Rais, kwani ameupiga mwingi kwa hatua hiyo inayogusa falsafa yake ya R4 yenye lengo la kuunganisha Watanzania bila kujali itikadi za vyama vyao.

Ninaamini kupitia maandamano hayo, dunia imeipata taswira ya Rais nn Samia kama mwanademokrasia na pia mwanasiasa mkomavu.

Ameonyesha ambavyo yuko tayari kuwavumilia viongozi wa vyama vya siasa kutumia haki yao ya kidemokrasia ya kuandamana kuonyesha hisia zao.

Rais ametegua kitendawili kilichokuwapo kwa muda mrefu kwamba maandamano hayawezi kuruhusiwa, lakini matarajio yamekuwa kinyume.

**Ninaamini kwamba, CHADEMA wamefikisha ujumbe walioukusudia haya kama hautatiliwa maanani au vinginevyo, lakini kitendo cha kuruhusiwa kuandamana kinaonyesha umakini wa Rais katika uongozi.**

SAFU

## FIKRA MBADALA

# Kongole Samia kwa haki ya kuandamana



Pascal Mayalla

KITU chanye nguvu kuliko kitu chochote duniani ni imani. Ukiamini unafungulia milango ya nguvu fulani zilizoko ndani yako zinazoitwa 'willpower' ambazo ni nguvu za nafsi ambazo zina uwezo wa kufanya kila kitu.

Wengi imani zetu tumezielekeza kwenye imani za dini kwa kumwamini Mungu lakini imani ya kweli iko ndani yako kwa sababu binadamu wote wana u-Mungu ndani yao.

Hata Yesu alipokuwa anafanya miujiza, aliwaambia watu "ni imani yako ndiyo imekuponya".

Imani hiyo si lazima iwe ni imani ya Mungu Baba, The Almighty God, hata Allah, hata Yesu, hata Mtume, hata Buddha, hata Mizimu, hata Mlima, hata Mti, hata Jiwe, hata chochote unachoamini, alimradi unaamini, hivyo imani yako itatenda.

Sala yetu ya kuliombea Bunge, huwa tunasema "Mungu huweka serikali za mataifa", hivyo hata marais Mwalimu Julius Nyerere, Ali Hassan Mwinyi, Benjamin Mkapa, Jakaya Kikwete, John Magufuli na sasa Samia Suluhu Hassan, wote ni chaguo la Mungu kwa Tanzania.

Hivyo mimi nina Imani kubwa sana na Rais Samia kuwa ana uwezo wa kuleta haki zote zilizoporwa Tanzania, ikiwamo kutuletea katiba mpya.

Imani kwenye kitu haichipuki tuu kama uyoga, au kudondoka kama 'love at first sight', Wasukuma tunaita "Moyo wangu umekudondokea", imani inajengwa kwa kuainishwa kisha ndipo unaamini.

Humu JF kuna mtindo, ukimsifu kiongozi mkuu wa nchi, unanyooshewa vidole vya tuhuma za kufanya uchawa, hivyo nikisema mimi nina imani na Rais Samia kuwa anaweza, naomba niwatembeze kidogo, huyu Samia, nilianza naye wapi na nilianza nae lini, ili mwisho wa siku nikisema namuaminia, uujue msingi wa imani yangu.

Kama iliyo kwa urais wa Samia, hakuna mtu yeyote alijua kuwa kuna siku Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania anaweza kufa akiwa madarakani!, hivyo siku zote Makamu wa Rais alikuwa anateuliwa tu bila kumhesabia anaweza kuja kuwa Rais kwa sababu hakuna aliyewahi kufikiri Rais wetu anaweza kufa!.

Hivyo naamini hata wakati Samia ni Makamu wa Magufuli, hakuwahi kuwaza kuwa kuna siku Magufuli, maarufu kama JPM, anaweza kuitwa kwa Baba yake na yeye kuwa Rais wa Tanzania.

Kwa hiyo ilipotokea JPM akaitwa kwa Baba yake na Samia kuwa Rais wa Tanzania, watu wote wanajua imejitokeza tu, ni mipango ya Mungu.

Ukweli ni kwamba hakuna kitu chochote kinachotokea tu, wala hakuna bahati mbaya.

Kila kitu kinachotokea kina sababu hivyo ni lazima kitokee. Kuna watu wenye nguvu wamewezesha, walitoa kauli zenye nguvu ya kuumba, waliomwomba Mungu, wakamumbia Samia urais wa Tanzania awe rais na kweli.

Kwanza anza kuangalia ni lini watu walianza 'kumspot' Mama Samia. Mimi nilimspot mwaka 2010.

Nilisema Huyu mama ana nguvu sana Zanzibar na miongoni mwa wanawake wachache wa shoka kutoka Zanzibar. Ni Mjumbe wa CC (Kamati Kuu) na NEC (Halmashauri Kuu ya Taifa) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Baada ya kuhudumu kwa miaka 10 kwenye Baraza la Wawakilishi, sasa ameingia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania JMT, atapewa wizara muhimu kumwandaa ama kuwa Rais au Rais wa Zanzibar kisha atapewa bara au kuwa VP (Makamu wa Rais) mwaka 2015.

Bandiko hili ni la 2010, angalia tulisema nini kumhusu Samia na nini kilikuja kutokea. Ndani ya miaka mitano ya kuwa katika Baraza la Mawaziri serikali ya Muuungano, akiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais. Ndiye alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba.

Kutokana na nyadhifa hizo, nikasema: "Kilichopo sasa ni kumwandaa kuwa kwanza Rais wa Zanzibar kwa kumpumzisha Dk. Ali Mohamed Shein baada ya kipindi chake cha pili kumalizika, kisha 2020 aje urais wa Muungano. Ili hili lifanyike, itabidi CCM iachane na ule utaratibu wake wa ngwe mbili za urais, kwa sababu ya kusubiria 2025.

Baada ya Rais Samia kuupata urais wa Tanzania na kuja na falsafa yake ya 4R, tumempigia kelele sana kuhusu kuruhusu mikutano ya siasa na maadamano, hatimaye akaruhusu. Tukampongeza pasi na hodi, huondoka pasi kuaga. Kuzuiwa bila kifungu, kuruhusu bila kifungu.

Ni hisani ya Rais Samia. Haki kuhisaniwa hadi lini?

Hivyo kama maandamano ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) yamewezekana chini yake Rais Samia, huu ni uthibitisho wa uwezo wa Rais Samia kutenda haki.

Kwa mantiki hiyo, nina imani kabisa na Rais Samia kwa asilimia 100 zile haki mbili kuu zilizotolewa na katiba yetu, haki ya kupiga kura na haki ya kupigiwa kura, zilitolewa na ibara ya 5 na ibara ya 21, kisha zikaja kuporwa na ibara ya 39 na 63, Rais Samia ana uwezo kabisa wa kuzirejesha.

Kitu tunachotakiwa kukifanya ni tuvute tu subra. Kila jambo na wakati wake. Kwa vile mikutano na maandamano ni haki ya vyama, wao waendelee kukutana na kuandamana, muda muafaka wa haki hizo kutolewa ukiwadia, haki hizo zinatolewa.

**Mungu Mbariki Rais Samia atende haki bin haki.**
**Mungu Ibariki Tanzania**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Wizara ya Elimu, Utamaduni na Michezo irejeshwe



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

KWA mara nyingine Taifa linalia, watoto wake wanaandika matusi kwenye karatasi za mitihani!. Wanaandika lugha chafu kwenye mitihani inayowapima uelewa wao kwenye masomo!

Watoto wa Taifa wanatungiwa mitihani kupimwa uwezo wao, ili walimu waone ni wapi penye tundu wazibe na palipo na udhaifu wapaimarishe, lakini walengwa wanaona ni upuuzi, wanatukana!

Utadhani watungao mitihani wanafanya hivyo kwa ajili ya maslahi yao binafsi, kumbe wanafanya hivyo baada ya wao kutungiwa mitihani kama hiyo miaka ya zamani, lakini wakaandika ilivyotakiwa bila kutukana.

Walijibu maswali bila kutukana, na ndio hao leo ni walimu wakiwafundisha hao wanaojigeuza mahayawani na kuandika matusi kwenye karatasi za mitihani! Eeh Mungu tumekosa nini waja wako?

Taifa tujiulize tumekosea wapi mpaka kuwa na kizazi hiki kinachotukana hata kwenye karatasi zilizobeba maisha yao, tena bila kuogopa wala kuhofia mustakabali wao. Ni nini basi?

Mbona zamani hakukuwa na masuala kama haya, tena mwanafunzi aliyefeli na kukosa kuendelea na masomo ya juu, aliomba kurudia na kuruhusiwa ili angalau ajaribu bahati yake kwa mara nyingine.

Ukifuatilia baadhi ya wataalamu wetu wa sasa, watakwambia walilazimika kurudia darasa la saba walipokosa kuchaguliwa safari ya kwanza na walipofaulu walieka juhudi na sasa wanakula matunda ya juhudi hizo.

Nini kimetokea sasa? Tujiulize na kutafuta suluhu ya haya yanayotokea ambayo ni aibu si tu kwa watoto, wazazi na walezi wao, bali ni kwa Taifa kwa ujumla wake.

Malezi majumbani, malezi mitaani na malezi shuleni, pengine yana mchango mkubwa katika kadhia hii inayosababisha uozo wa kiakili, kwa baadhi ya wanafunzi ambao hata hivyo ni wachache, lakini samaki kaanza kuoza tengani.

Mitaani hivi sasa matusi ni lugha ya kawaida. Tunasikiliza nyimbo zikiimbwa na wanaojiita wanamuziki wa kizazi kipya, zikisheheni matusi ambayo nasi wazazi tunazishangilia na kuwapongeza kwa kuwa wanamuziki nyota.

Waimba matusi hao ni kizazi cha vijana kilichofanikiwa kimaisha, na kusujudiwa na sisi wazazi na walezi wao, tunawachukulia kama vipenzi wahamishaji wa kisiasa na kukumbatiwa na wanasiasa!

Watoto walioko shuleni wanatamani kuwa kama wanamuziki au wasanii hao, ambao wengi wao ni waliofeli masomo na kuingia kwenye fani hiyo, hivyo kuwaona kama 'role models' wao kimaisha, kwamba hata wakitukana wanabaki kuwa watakatifu tu kimaisha.

Kama ndivyo, kwa nini mtoto asiandike matusi kwenye mtihani wake na kuwa na uhakika wa kufeli, ilhali akijua kuwa muziki wa kizazi kipya unamsubiri mtaani ili 'atusue' kimaisha?

Hebu kosea mathalan hivi sasa uende kuliko na starehe ya burudani ya muziki wa kizazi kipya hususan kwenye baa, usikilize nyimbo zinazoimbwa huko na kushangiliwa na walevi mchanganyiko wa wazee na vijana!

Si huko tu, jaribu kwenda kwenye sherehe za harusi usikilize nyimbo za kizazi kipya kama hujasikia matusi ya nguoni na masuala yanayohusisha faragha, lakini leo ndiyo yanaimbwa hadharani!

Sikushangaa siku ambayo nchi ilitembelewa na Rais wa nchi jirani, jukwaani akapandishwa msanii wa kizazi kipya mbele ya marais hao wawili; mwenyeji na mgeni wake, akaimba wimbo ambao kwangu mimi si wenye staha!

Lakini alishangiliwa na kila aliyekuwa pale wakiwamo wakuu wa mataifa hayo mawili, ambao najua hawakuwa wanaelewa kinachoimbwa, bali kupiga makofi kwa sababu wengine walishangilia!

Msanii huyo aliyeimba alichoimba, akatoka hapo bichwa kubwa na mfuko umefurika minoti ya kutuzwa, achilia mbali mamilioni ya kumkodi kuburudisha hadhira ile ya ujio wa mgeni wa kimataifa.

Kama wewe ni mtoto unasoma shule ya msingi au sekondari na unaona maisha ya wanamuziki wa kizazi kipya waliofeli shule na kufanikiwa kimaisha kwa kuimba matusi, utachagua wapi?

Wizara yenye dhamana ya utamaduni wa Taifa hili ipo. Inafanya nini? Hakika ndiyo inayoiumiza Wizara ya Elimu, kutokana na wasanii wake. Mkikubaliana na mimi, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ivunjwe na iunganishwe na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Kufanya hivyo kutasababisha Waziri wa Elimu, Utamaduni na Michezo (wizara mpya), asimamie vyema maadili ya wanafunzi na wasanii na wanamichezo, lakini pia atasaidia kuibua vipaji kwenye michezo tofauti na ilivyo sasa.

Ikumbukwe, Wizara hiyo ilikuwapo zamani ikisimamia vyema dhamana yake na tukapata wanamichezo wengi nguli na hakukuwa na matusi kwenye mitihani. Nini kitashindikana sasa?

**Asalamaleko!**

# 335 watiwa mbaroni msako wiki moja, wamo watuhumiwa mauaji

**Na Rose Jacob,** MWANZA

OPERESHENI iliyofanywa na Jeshi la Polisi mkoani Mwanza kwa kipindi cha wiki moja imewatia mbaroni watu 335 kwa tuhuma mbalimbali zikiwamo za mauaji, uhalifu, wizi, matumizi na usafirishaji wa dawa za kulevya na uhamiaji haramu.

Idadi kubwa ya watuhumiwa wametajwa kukamatwa katika maeneo ya wilaya za Nyamagana, Ilemela na Magu. Kati yao, 133 wamefikishwa mahakamani na wengine 202 uchunguzi unaendelea.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilbroad Mutafungwa alibainisha kuwa jumla ya watuhumiwa 335 walikamatwa katika oparesheni hiyo, wakiwamo watuhumiwa 51 wa dawa za kulevya, 17 wanaodaiwa kuvunja nyumba na kuiba, 13 wana tuhuma za mauaji, 47 wanadaiwa kufanya vitendo vya uhalifu na watano wanaodaiwa ni wahamiaji haramu kutoka Burundi.

"Pia tumekamata vidhibitisho mbalimbali zikiwamo simu zaidi ya 50 za mkononi zilizoibwa katika maeneo mbalimbali mkoani hapa, kompyuta, redio, televisheni, vifaa vya kutengeneza simu na hii ni kufuatia taarifa kutoka kwa wananchi wasiopenda uhalifu, wakaguzi kata pamoja na uchunguzi kupitia watoataarifa fiche," alisema.

Kamanda Mutafungwa alisema kuwa hadi sasa watuhumiwa 133 wameshahojiwa na kufikishwa mahakamani huku wengine 202 hawajahojiwa na taratibu zinafanyika ili watuhumiwa wote wafikishwe mahakamani kwa ajili ya taratibu zingine za kisheria.

"Niwaombe wananchi wanunue simu na vitu vingine katika maeneo rasmi ili kujiepusha na kuuziwa vitu vya wizi. Pia tutakwenda kushirikiana na TCRA (Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano nchini) ili kubaini matapeli wote wa mtandaoni," alisema.

Pia aliwataka wakazi mkoani hapa kufika katika vituo vya polisi wilaya za Ilemela na Nyamagana kwa ajili ya kutambua vifaa vyao ili kusaidia pia katika uchunguzi wa jeshi hilo.

Kamanda Mutafungwa aliwataka wananchi kuwa watulivu wakati wote kwa kuwa hali ya usalama iko vizuri. Pia wajiepushe na matukio ya uhalifu kwa kuwa ni kinyume cha sheria.

Aliwakumbusha wenyeviti wa mitaa kuendelea kufuatilia na kutoa taarifa juu ya vijana wanaojihusisha na matumizi ya dawa za kulevya ili kuliwezesha jeshi kuwachukulia hatua stahiki na kuitaja operesheni hiyo kuwa endelevu.



Katibu wa Umoja wa Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Dar es Salaam, Iddy Mvano akizungumza katika kikao kazi cha kufuatilia uhai na utekelezaji wa jumuiya hiyo, katika kata ya Kisukuru, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto kwake ni Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya Wazazi mkoa, Salum Kibanda na Muhamad Sadik. **PICHA: MUHIDINI MSAMBA**

## TGNP yawakumbusha utu, usawa ugawaji rasilimali

**Na Zanura Mollel**

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP) umeshauri viongozi wanawake nchini kuzingatia utu na usawa katika ugawaji wa rasilimali kwa makundi yote.

Mkurugenzi Mtendaji wa mtandao huo, Lilian Liundi, alitoa ushauri huo alipokuwa akiongea kwenye mafunzo ya siku 10 yanayotolewa jijini Dar es Salaam kwa wanawake (feminists) kutoka katika nchi za kanda ya Afrika.

Alisema mafunzo hayo yanatekelezwa kwa kushirikiana na wadau kutoka taasisi ya COADY iliyopo nchini Canada, na pia taasisi hiyo imewezesha mradi wa miaka mitano utakaogusa maisha ya wanawake wa Kitanzania.

Alisema, lengo la mafunzo hayo ni kubadilishana uzoefu wa masuala ya kijinsia na uongozi kwa mwanamke pamoja kudhibiti dhana ya ukoloni katika harakati za wanawake kwa kufanikisha usawa wa kijinsia pamoja na kuzingatia haki za binadamu.

"Nchi mbalimbali zimeshiriki ikiwamo wawakilishi kutoka katika serikali za nchi husika, mashirika binafsi pamoja asasi za kiraia, baadhi ya nchi hizo ni Afrika Kusini, Kenya, Uganda, Serilione, Canada, Cameroon," alisema Liundi.

Aidha, alifafanua kuwa wamejipanga kuangalia, kujadili hali ya utekelezaji na mgawanyo wa haki sawa kwa makundi maalum, ikiwamo watu wanaoishi na ulemavu, vijana, wanawake wa mijini na vijijini, wanaume wagonjwa na wale waishio vijijini na mijini.

"Matamanio yetu ni kuona uongozi unaoangalia utu na siyo vitu, kwa kuzingatia mgawanyo wa haki sawa na fursa mbalimbali kwa makundi yote hapa nchini," alisema Liundi.

Mkurugenzi wa Gloring Feture Tanzania yenye Makao Makuu jijini Dodoma, Aisha Msantu, alisema kuwa mafunzo hayo ni mkombozi kwa makundi maalum, ikiwamo watu wanaoishi na ulemavu kwa kujengewa uelewa wa kushiriki katika chaguzi kwa kuwania nafasi za serikali za mitaa 2024 pamoja na uchaguzi mkuu mwaka 2025.

Naye, Anna Marwa kutoka taasisi ya PELUM-TZ alisema matarajio yake ni kuona vyama vya siasa vikitanua wigo kwa kuongeza nafasi za ushiriki wa wanawake katika nyanja za utoaji wa maamuzi.

Aidha, alifafanua kuwa mafunzo hayo yatawajengea uelewa washiriki kuhusu masuala ya uongozi kwa wanawake na wanatarajia baada ya mafunzo hayo kuanza kutoa elimu kwa wanawake kushiriki katika chaguzi za serikali za mitaa 2024 zinazotarajiwa kuanza nchini.

Eris Smith, Meneja Programu, uongozi wa wanawake na uraia hai wa Taasisi ya COADY yenye makao yake makuu nchini Canada, alisema wamepongeza utekelezaji wa mpango huo na TGNP ambayo yatasaidia wanawake wa Kiafrika kuleta mabadiliko na kutoa changamoto kwa mifumo na miundo hasi inayoathiri jamii.

"Kwa kweli tuna furaha kutoa kozi hii na TGNP inayowaleta pamoja viongozi kutoka duniani kote ili kuchunguza na kufunua mambo muhimu kwao na kupinga mifumo na miundo hasi inayoathiri maisha yetu," alisema.

Katika hatua nyingine, alifafanua kuwa umuhimu wa mpango huu ni kuwaleta pamoja watu kutoka nchi zote zinazoendelea na wengi kote barani Afrika na kuhakikisha kwamba uelewa tofauti wa ufeministi, uondoaji ukoloni na uongozi wa wanawake unaweza kufunguliwa pamoja na kuchunguzwa ambapo tunaweza kujenga uelewa wa pamoja na mshikamano.

## Tanzania yaanza uenyekiti wa mikutano ya AfCFTA

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI ya Tanzania imeanza kuwa Mwenyekiti wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) kwa muda wa mwaka mmoja wa 2024.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdalah ndiye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maofisa Wakuu wa Biashara katika vikao vya AfCFTA.

Tanzania ilichaguliwa kuwa mwenyekiti wakati wa kongamano la wanachama wa mkataba huo hivi karibuni katika kongamano la AfCFTA lililofanyika kwenye Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam.

Akifungua mkutano wa 16 wa Kamati ya Maofisa Wakuu wa Biashara wa AfCFTA, jijini Durban, Afrika Kusini, Dk. Abdalah alisema nchi wanachama wa mkataba huo wanapaswa kushirikiana kwa usawa kurekebisha sera zinazowezesha kuchochea ukuaji uchumi wa nchi hizo.

Alisisitiza sera hizo zinazotungwa zinapaswa kuondoa vikwazo, kukuza ushirikishwaji na kuhakikisha faida za AfCFTA zinafika pembe zote za Bara la Afrika.

"AfCFTA inawakilisha ishara ya matumaini na fursa, inatufunza katika maono ya pamoja ya kukuza maendeleo endelevu kupitia biashara imara ya ndani ya Afrika," alisema Dk. Abdallah.

Vilevile, alibainisha kuwa kamati hiyo ina jukumu muhimu katika kuonesha ufanisi wa utekelezaji malengo ya AfCFTA kwa kushiriki katika mazungumzo ya wazi yanayolenga yaliyo bora kwa Afrika kwa ujumla, badala ya nchi binafsi.

"Tunapofanya majadiliano ya kina, tuwe na mtazamo mpana wa Afrika, tukizidi nchi zetu binafsi, tukitambua kuwa kila uamuzi tunaoufanya una uwezo wa kuathiri maisha ya mamilioni ya watu. Ni jukumu letu la pamoja kuhakikisha kuwa athari hizi ni nzuri, za usawa na endelevu," alisisitiza Dk. Abdallah.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha (Usimamizi na Uchumi), Elijah Mwandumbya, alisema mkutano huo unalenga kutatua masuala ya kikodi ili kurahisisha biashara katika Bara la Afrika.


MAISH
JANUARI 28, 2024
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jun



# MWENDO WA BWANGA

Ukurasa 13

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 4 | 0 | 2 | 1 | 7 | 0 | 5 | 2 | 8 | 3 | 2 | 8 | 3 |
| 0 | 1 | 8 | 7 | 6 | 2 | 4 | 6 | 6 | 4 | 9 | 6 | 6 |
| 7 | 7 | 1 | 4 | 7 | 9 | 9 | 0 | 0 | 5 | 5 | 7 | 4 |
| 3 | 5 | 1 | 1 | 7 | 0 | 8 | 2 | 0 | 8 | 0 | 7 | 5 |
| 9 | 9 | 7 | 8 | 4 | 2 | 8 | 6 | 0 | 4 | 9 | 5 | 3 |
| 1 | 3 | 9 | 3 | 9 | 0 | 0 | 6 | 6 | 8 | 2 | 6 | 0 |
| 1 | 7 | 2 | 7 | 7 | 6 | 5 | 8 | 1 | 3 | 0 | 4 | 0 |
| 7 | 6 | 8 | 7 | 9 | 6 | 1 | 0 | 6 | 9 | 8 | 4 | 9 |
| 9 | 3 | 0 | 6 | 6 | 5 | 1 | 6 | 5 | 2 | 4 | 7 | 7 |
| 1 | 4 | 1 | 8 | 8 | 6 | 6 | 1 | 7 | 9 | 3 | 7 | 6 |
| 0 | 3 | 9 | 3 | 5 | 5 | 3 | 7 | 8 | 5 | 7 | 7 | 0 |
| 5 | 1 | 2 | 5 | 2 | 7 | 7 | 9 | 0 | 6 | 9 | 1 | 3 |
| 6 | 6 | 5 | 8 | 2 | 3 | 3 | 9 | 2 | 6 | 9 | 1 | 4 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | ■ | U | S | I | K | U |
| A | ■ | ■ | ■ | G | ■ | C |
| T | ■ | B | A | I | ■ | H |
| E | D | A | ■ | Z | O | A |
| N | ■ | N | A | O | ■ | C |
| D | ■ | D | ■ | ■ | ■ | H |
| O | K | O | K | A | ■ | E |

## FUMBO TOTO


| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | ■ | | | | | |
| | ■ | ■ | ■ | | ■ | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | | | ■ | | | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | ■ | | ■ | ■ | ■ | |
| | | | | | ■ | |

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


GAO, MKE, EDA, MEI, OBAMA, AKOME, NDANI, GAMBA, MAGENDO, INGIZWA

## AMSHA AKILI

STOO YETU IMEVAMIWA NA PANYA 23, HEBU WATAFUTE TUWATIMUE!




## TOA TOFAUTI 5



## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

MTOTO Peter alikuwa akimsaidia mama yake kumwagilia maji maua katika bustani iliyopo mbele ya nyumba yao.

Wakati wakiendelea kumwagilia maji Peter alimuuliza mama yake kuhusu tabia ya nyuki kupenda maua.

Peter: Eti mama kila kwenye maua kuna nyuki?

Mama: Ndio mwanangu, ni lazima nyuki watakuwa karibu na maua?

Juma: Kwani kila ua lina nyuki wake? Mbona mwalimu alituambia kila nyuki hufuata ua lake?

Mama: Hapana huo ni msemo unaomaanisha kila zuri linatokana na chanzo chake.

**SWALI**

**Taja matumizi tofauti ya chakula aina ya karanga**

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Chanzo cha ndoa nyingi kuishia njiani!

KARIBU tena msomaji wangu tuendeleze mada zetu za Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki iliyopita nilileta hapa mada kwamba ndoa ni taasisi isiyokuwa na mzoefu au mwenyeji.

Pia nikasema kwamba ndoa ni taasisi ambayo haina kufuzu na kwamba kama ukimweka Mungu pembeni hata kwa dakika moja, kila kitu kitaharibika.

Ni taasisi inayopingwa sana na shetani na mawakala zake kuliko taasisi nyingine yoyote maana anajua akishavuruga ndoa, familia jamii, nchi na hata ulimwengu utaathirika.

Pamoja na ukweli kwamba ndoa nyingi zinafungwa kila mwaka, vivyo hivyo, ndoa nyingi zinaishia njiani kwa sababu mbalimbali, mvurugaji mkubwa akiwa ni shetani.

Utafiti uliowahi kufanyika uligundua kuwa wanawake wengi hawafurahii ndoa zao. Pale wanapoanza kuchukua maamuzi kufurahia ndoa zao, maisha ya waume zao hukatishwa. Wanapopata mbinu kurejesha ndoa zao, tayari waume zao wanakuwa wameshakufa.

Imekuwa hivyo kwa sababu wanawake wengi sana wamejiingiza katika maagano mazito ya kuzimu kwa madai kuwa wanatafuta msaada wa ndoa zao kwa waganga, pasipo kufahamu kuwa ni shetani anawashambulia.

Ni ukweli usiopingika kuwa shetani anajua kuwa kama akifanikiwa kuteka jamii ya wanawake, basi ataitawala dunia. Ingawa wanawake wanaitwa viumbe dhaifu, lakini majukumu waliyopewa hayawezi kufananishwa na msingi wa neno hili.

Hata kama mwanamume akiwa mtu mkuu sana katika maisha yake, ni lazima ajue kuwa kuna wakati alikuwa kichanga katika tumbo la mwanamke. Shetani anajua kuwa mwanamke anatawala/anamiliki uzao (tumbo la uzazi), chimbuko (chanzo cha asili) na pia anatawala jiko. Ukitafakari maneno haya matatu, utagundua kuwa mwanamke anatawala ulimwengu katika vitu hivyo vitatu hapo juu.

Shetani pia anafahamu ukweli kuwa akiwaachia wanawake wawe na bidii ya kumtafuta Mungu na wamiliki maeneo muhimu katika historia ya dunia watatikisa ufalme wake. Hivyo wanawake wana vita kali ya kupigana na shetani. Na uadui kati yao una mizizi mirefu.

Ndiyo maana neno la Mungu linasema, "nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake, utakuponda kichwa na wewe utamponda kisigino".

Katika mpango wa Mungu kutukomboa, mbegu ya mwanamke ambayo ingemkanyaga kichwa, shetani ameamua kushambulia kila mwanamke kwa sababu hajui ni mwanamke yupi anaweza kuzaa mbegu hatari kwake.

Kwa hiyo alianza mipango yake dhidi ya wanawake kwa kupotosha, kuchafua, kuwashushia hadhi na kuwafanya wanawake wadharaulike katika jamii.

Kama wanawake wangejua wako chini ya vita kali kama hii, wangeacha kubaki katika hali ya ulimbukeni(ujinga) na kuanza mashambulizi makali dhidi ya adui yao shetani.

Wakati umefika sasa kwa wanawake kusimama na kumpiga huyo adui msumbufu. Kila mwanamke anatakiwa kusimama katika nguvu na uweza wa Mungu kumiliki kilicho halali yake.

Msomaji wangu, nimetoa elimu hiyo hapo juu kujaribu kuonyesha kwa nini wanawake wanavurugwa sana kwenye ndoa. Ukienda kwenye mahakama zetu, wanawake wengi wamekimbilia mahakamani kudai talaka.

Ndoa zinafungwa vizuri maisha yanaanza vizuri, lakini pale wanandoa wanapoanza kufurahia maisha, tena baada ya kujaliwa kupata mtoto/watoto, ndipo shetani huzusha majaribu kuwavuruga.

Shetani haonekani kwa macho kwani ni roho. Hutumia watu kama mawakala wake. Wanaweza kuwa waganga wa kienyeji. Au ndugu wa karibu, jirani, rafiki, kwani maandiko ya Mungu yanasema, adui wa mtu ni wa nyumbani kwake.

Nyakati hizi shetani anashambulia sana ndoa changa. Wengi hawajapata hata mtoto lakini tayari wanandoa wana mgogoro au hata kutengana. Sababu zingine ni za kijinga kabisa hazina mashiko lakini ndio hivyo ndoa zinayeyuka.

Yuko binti mmoja aliolewa ndoa nzuri sana mwezi Mei mwaka jana. Yeye na mumewe wote wameokoka. Send-off ikafanyia Dar kisha ndoa ikafanyikia Mwanza anakoishi kijana. Binti mwenyeji wa Kilimajaro.

Ghafla nikamuona binti Dar mwezi Septemba, miezi mitano tu baada ya ndoa. Nilipodadisi hivi majuzi kujua mbona binti yupo Dar muda bila mumewe, jibu likawa wametengana.

Kisa eti wazazi wa kijana hawakutaka aoe mwanamke wa kabila tofauti na wao. Wanataka Msukuma mwenzao siyo mgeni. Swali ni je, kwanini waliridhia ndoa ifungwe wakati hawampenda binti wa kabila lingine?

***Msomaji wangu kwa leo niishie hapa, Je, una maoni, Kisa? Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Misimamo mapenzi jinsia moja, imemwogopesha

KUNA kelele nyingini mitaani, watu wameamka. Si maaskofu wala mashehe, wote sauti ni moja tu, hatuutaki.

Kashfa kuhusu baadhi ya Watanzania kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja na kuweka hadharani haiba yao ni kama inaanza kuzoeleka.

Kama taifa, jambo hili tusipoweka nguvu kulidhibiti na kulichukia, litachukua miaka kadhaa, kukubali au kutokubaliana na hali hiyo.

Ndiyo! nimemsikia Mkuu mpya wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Malasusa akitangaza kama msimamo wa Kanisa kuukataa.

Nimelisikia Baraza la Maaskofu la Kanisa Katoliki Tanzania (TEC), wakiweka wazi msimamo wao wa kutounga mkono mapenzi ya jinsia moja. Vivyo hivyo, kwa baadhi ya mashehe wa Baraza la Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA).

Maana yake vita hii ya mtu mmoja moja. Ni kwa sababu inaonekana kuna mahali tulijisahau na kuacha mizizi kuota na uamuzi wa kupambana nalo unakwenda taratibu.

Najiuliza kwa yanayotajwa kuendelea nchini kuhusu ushoga na usagaji; Je tunahitaji msaada wa wataalamu wa 'Forensic Psychology', yaani uchunguzi wa kina wa saikolojia ya jinai kuwabaini wanaovuruga maadili yetu kama Watanzania au tuendelee kutumia sheria zile zile?

Kwa nini? Sababu ya kwanza ni kwamba forensic psychology pamoja na mambo mengine inashughulika pia na saikolojia ya uhalifu, ambao kwa maana nyingine ni utafiti wa wawazo na matendo ya wakosaji.

Kimsingi, forensic psychology inatoa jibu kwa swali la kwa nini wahalifu hufanya kile wanachofanya.

Kama ndivyo, ifike mahali ili kupamba na watu hawa kisawa sawa, ni lazima tutengeneze wanasaikolojia wa maisha halisi mitaani, kwenye maeneo ya starehe na maeneo ya huduma kama shule na kadhalika, ambao hawezi kuandamana na maofisa wa Polisi kukabiliana na washukiwa.

Hawa kwa kuzingatia ujuzi wao wa tabia ya binadamu, hasa kwenye eneo la jinai dhidi ya saikolojia ya uchunguzi, wanaweza kwa mfano, kuwasaidia maofisa wetu kutoa taarifa za wanaoendesha biashara ya mapenzi ya jinsia moja; na vilevile katika kuuliza maswali yanayofaa wakati wa kuhojiwa au kutoa mambo muhimu ili kusaidia uchunguzi wao. Jambo baya zaidi, huko katika Jiji la Arusha kama tunaambiwa hali ni mbaya, kwa kuwa inakadiriwa vijana 4,000 wanajihusisha na mapenzi ya jinsia moja. Je mikoa mingine, hali ikoje? inawezekana ikawa ni zaidi ya Arusha.

Ziko taarifa za kuaminika ambazo zinaeleza kuwa baadhi ya maeneo ambayo yanatajwa kushamiri kwa vitendo hivyo katika jiji hilo ni Vituo vya Makuzi ya Watoto (Day Care) na baadhi ya taasisi za kiraia (NGO) ambazo zinaomba usajili kwa minajili ya kutoa elimu kwa jamii.

Kwamba, kuna taasisi nyingine zinakuja kwa mgongo wa kutoa elimu kwa wananchi, kumbe zinakuja kuratibu masuala ya ushoga kupitia Day Care na katika vituo vya taasisi zao.

Niliwahi kuandika kataa utamaduni wa magharibi unazotweza utu, nikimaanisha vita inayoendelea sasa ya ushoga, usagaji ni masuala yanayochochewa na mabadiliko ya kijenetiki, ambayo huchochea tabia ya kutweza utu.

Ni kwa sababu, utu wa mwanadamu umegawanyika katika aina tatu za utu, yaani introvert, extrovert na ambivert.

Kwa ufupi sana, hili la mapenzi ya jinsia moja ndio haswa linaloguswa katika aina ya ambivert, ambayo inatumiwa sana na watu hawa tunaowakataa katika jamii kutokana na hulka yao na mienendo yao katika kuharibu taifa la Mungu.

Ni lazima Watanzania wajue kwamba, utu ni mchakato wa muda mrefu, ambao huanza na kuzaliwa na kuendelea katika utoto hadi ukubwani.

Kwa sababu, utu una jukumu muhimu sana katika tabia ya binadamu, tukatae tamaduni za magharibi zinazotweza utu!


Bunge letu kuagiza serikali, kufanya utafiti wa kina kuhusu ukubwa wa tatizo la ushoga au mapenzi ya jinsia moja hapa nchini, na mambo gani ambayo taifa linataka kwa wakati huu,

Yaongezeke kwenye Sheria ya Makosa yaKujamiana (SOSPA) ya Mwaka 1998 na Sheria ya Kanuni ya Adhabu (Penal Code), ni hatua kubwa katika vita hii.

Kwa sasa sheria zetu zinasema hata kukubali tu kuingiliwa kinyume na maumbile, ni kosa, na ni kinyume na kifungu 154 (1) (c) cha Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria iliyofanyiwa Marejeo ya Mwaka 2022.

***•Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI





Hivi ndivyo Haji Manara na Zaylisa walivyofunga ndoa ya kimya kimya hivi karibuni





# MITINDO





## MWENDO WA BWANGA

SURUALI pana maarufu kama 'bwanga, zimenza kutumika kwa miaka mingi na hadi leo zinaendelea kupendwa na watu wa rika zote.

Ni jambo la kawaida kuwaona watu maarufu duniani kama wasanii, wanasiasa na wanamichezo wakiwa wamevaa aina hii ya suruali wakiwa katika hali ya kuvutia zaidi.

Kwa ujumla suruali za bwanga au katika tasnia ya mavazi inaitwa Pallazo pants ndizo zinaongoza kwa kuendelea kupendwa zaidi kwa karne nyingi kuliko aina nyingine za nguo.

Aina hii ya mavazi hutengenezwa kwa aina mbalimbali za vitambaa kama vitenge, batiki, vikoi, jeans , polista na nyinginezo.

Kwa miaka yote wabunifu wamekuwa wakitumia vipaji vyao kuvumbua aina mbalimbali ya suruali za aina hii na kusababisha kila siku kuonekana kuwa ni mpya.

Wataalamu wa mavazi wanasema aina hii ya nguo inaendana na mazingira yoyote hasa kutokana na sifa yake kuu ya kutunza mwili katika kukabiliana na joto au baridi kwa kufuata ushauri maalumu.

Wanasema kimsingi mwili unatakiwa kuwa huru katika hali yoyote kama kutembea au kukimbia, hivyo bwanga inatoa uhuru kwa mtu husika kufanya hivyo.

Suruali ya bwanga inaendana na aina nyingine za nguo zinazoambatana, kwani inafaa kuvaliwa kwa fulana, shati la mikono mirefu au mifupi, blauzi na fulana zile za kubana.

Upande wa miguuni hapo itakuwa chaguo lako pekee kwani ukivaa raba, viatu vya visigino virefu au vifupi, sando au viatu vya ngozi, hapo utakuwa umeshaini.

UREMBO

Na Mary Geofrey

# Unatokaje na kucha safi za miguu?



IDADI kubwa ya wanawake hawazingatii sana usafi wa kucha za miguuni kama ilivyo kwa mikononi. Tabia hii si kitu cha ajabu kuta mtu ana kucha ndefu.

Kucha za miguu ni muhimu sana na zinahitaji utunzaji makini.

Ingawa kucha za miguuni huwa zinafichika kutokana na kuvaa viatu na soksi, lakini muhimu tujifunze namna ya kukata kucha kwa usahihi.

**Namna ya kukata kucha**

Andaa kucha kabla ya kuzikata: kabla ya kuanza kukata kucha ni muhimu kafanya maandalizi.

Kwanza lazima tuziloweke kwa angalau dakika 15 katika maji ya joto yenye chumvi ili ziwe laini na rahisi kukata.

Jinsi ya kukata kucha za miguu ni lazima ujue kucha zinakatwa kila wakati na kuwekwa kwenye sura ya mraba.

Kumbuka kuwa pembe za kucha hazipaswi kuwa fupi sana kuzizuia kukua ndani ya ngozi ya kidole.

Tumia mkasi au kiwembe katika ukataji wa kucha kwa kuziweka katika umbo linalopendeza.

Ukishapata kucha fupi, tenganisha kila kidole chako na mpira wa pamba. Kisha paka polishi ya wazi na iache ikauke kabla ya kupaka rangi ya pili.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Furahia mbuzi choma

WATU wengi wamezoea kula nyama ya mbuzi ya kuchoma kwenye maeneo ya starehe au migahawa kwa sababu inakuwa laini na nzuri.

Katika safu hii wiki hii tunaelezana njia rahisi za kuchoma nyama ya mbuzi ukiwa nyumbani na kufurahia maisha.

Unahitaji uwe na vitu vifuatavyo ili kukamilisha kuchoma mbuzi wako.

Miongoni mwa vitu hivyo ni vitunguu swaumu vilivyosagwa, tangawizi iliyosagwa, mafuta kiasi cha nusu lita na beef masala.

Mahitaji mengine ni chumvi kiasi kidogo maana nayo ikizidi sio nzuri, pilipili, mkaa na mbuzi ambae tayari amesha kutolewa uchafu wa tumboni

Namna ya kuandaa

Jinsi ya kutengeneza jiko lako kwa ajili ya kuchoma mbuzi wako

Chukua celery, unachanganya swaumu, mafuta, tangawizi, chumvi na beef masala na ziache kuwa muda nyama ilainike.

Baada ya hapo unatengeneza sehemu nzuri ya kuchoma kuna wengine wanatumia majiko yale ya kuokea nyama wengine wanatumia majiko ya asili.

Unaweza kutumia njia ya kienyeji kwa kuchimba sehemu unaona hapatakusumbua kuchomea mbuzi wako na akaiva vizuri.

Ukishaandaa jiko lako na mkaa unaweza kuweka nyama yako na kuanza kuchoma.

Utachoma mbuzi wako taratibu kwa moto wa wastani hadi hapo utakapoona ameanza kuiva.

Ukiona maeiva vyema na kuwa tayari kuliwa unaweza kumkatakata vipande na ukamtenga mezani kwa ajili ya kuliwa.





MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Panga ratiba ya usafi wa nyumba uiimarishe

UCHAFU unachangia kwa kiwango kikubwa kuharibu nyumba hata kama ni nzuri na iliyojengwa katika uimara kiasi gani.

Mwingine anaweza kusema kwamba mbona kusafisha nyumba ni jambo linaloeleweka, lakini ninachotaka kueleza ni kwamba ni namna gani unatakiwa kuweka kipaumbele na kujiwekea ratiba nzuri ya usafi wa nyumba yako yote.

Kumbuka kwamba nyumba ikisafishwa kwa umakini na ufasaha ni dawa inayojitosheleza katika kuiimarisha na ikadumu zaidi kama ambavyo ni kinyume kwamba isiposafishwa vizuri ina uwezekano mkubwa wa kuharibika na kupoteza mvuto na uimara wake.

Jambo la msingi na la kuzingatia ni kwamba nyumba ina maeneo mengi na kila eneo linahitaji kusafishwa kwa umakini kwa ajili ya ustawi wake.

Ili ufanikiwe katika hilo ni lazima kujiwekea utaratibu mzuri wa kujipangia ratiba ya namna gani bora ya kufanya usafi katika kila eneo la nyumba yako.

Kwa mfano kama ni jikoni, chumbani, sebuleni, jikoni, nje ya nyumba, stoo, vyooni na katika viunga vyote vya nyumba hakikisha kwamba kote kunafanyiwa usafi wa uhakika kila mara.



Kwenye maeneo yote ya wazi yakiwamo yale yanayohitaji kufagiliwa, hakikisha unafanya hivyo, kama umepanda maua, yahudumie nayo vizuri kwa kuyawekea mbolea na kuyamwagia maji pamoja na kuyatengenezea mazingira ya kuendelea kustawi zaidi na yasigeuke kuwa uchafu kwenye nyumba.

Baada ya kufanya usafi hakikisha unakagua kila eneo la nyumba ili kujiridhisha kama endapo kila mahali kumeguswa na usafi na kama kuna vitu ambavyo havihitajiki au havitumiki, viondoe.

Na baada ya kusafisha hakikisha kila kitu kwenye nyumba kimepangiliwa inavyostahili kuanzia jikoni, sebuleni, vyumba vya kulala, vyooni na hata nje ya nyumba kwenye bustani na sehemu nyinginezo.

Hakikisha kwamba yale maeneo yote ambayo yanahitaji kufanyiwa usafi kila siku inafanyika hivyo na usafi kwenye kila eneo la nyumba yako ndio utaiimarisha lakini endapo hakutakuwa na mpango mzuri wa kuisafisha utaiharibu.

## DONDOO

# Zijue nakshi za milango mikubwa

Na Restuta James

MABADILIKO ya nyanja mbalimbali na hasa ya kiteknolojia yamerahisisha upatikanaji wa taarifa hususani za kibunifu, hivyo kuongeza wigo wa maarifa kwa watu wa sekta zote.

Hii imerahisisha pia ubunifu wa ujenzi na makazi pamoja na mandhari nzima ya nyumba.

Fundi seremala, Gabriel Massawe, anasema teknolojia imewasidia kuboresha kazi za ufundi kuanzia samani za ndani, mitindo ya jiko, milango, vitanda, makabati na meza za matumizi tofauti tofauti.

Akiangazia milango anagusia mikubwa ya mbele ambayo inabuniwa kwa namna ambayo inapaswa kufungwa bila kuweka mlango wa chuma (gril).

"Mwonekano wa mlango wa mbele unapaswa kuwa wa kipekee na tunashauri kama mtu anaweza aweke milango imara ya mbao za mninga au mkongo," anasema.

Anasema milango mikubwa inaweza kunakishiwa kwa mbao na vioo ili kuleta mwonekano bora zaidi au kuacha mbao 'iongee' kwa kutoiwekea kitu cha nyongeza zaidi ya michoro.


Anasema kwa wapenzi wa vioo, sio lazima viwekwe kwenye milango moja kwa moja bali kinaweza kuwekwa kama mbadala wa tofali kwenye ukuta unaoshikilia mlango.

"Kama milango unayoiona (huku akionesha picha kwenye simu), mingine ni mbao plain, mingine ina maua kama hivi na wengine wanapendelea kioo, sisi tunashauri watu wasiweke magrili kwenye milango," anasema Massawe.

Anashauri kuwa milango hasa ya kutoka nje ina nafasi kubwa katika kuboresha mwonekano wa nyumba hivyo watu wazingatie kuhakikisha ina mwonekano mzuri.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
'HUU UGONJWA WA MACHO JAMANI HAUKIMBILIKI KAMA 'MKOPO WA BENKI'
PASUA BABAAA HAHAAA
JUKWAANI
MKIBADILI MANENO YENU... NA SISI TUTABADILI VITENDO VYETU... UKINISINGUA, NAKU-SINGUA TUNASINGUANA
'LONG'TAIMU AGOO... HIZI NDIO PIGO ZANGU MIWANI UA GIZA INANITOA CHICHA
WEWE BHANA USHA-KWAMA!
WEEWEEEEE!!!
NILIKUJA MGUU UNAUMA 'MKANIKATA' NIKAJA TENA MENO YANAUMA MKAYA-NG'OA! ...LEO MACHO...?
PIA TUTAYA-NG'OA
HUU UCHURO KABISA NDIO MAANA NIMEKOSA KUHOJIWA 'NIKIWA WODINI NITOKEE KWENYE TIVII
KWA HIYO ULIKWENDA KUANDAMANA 'UBONDWE' UTOKEE KUNAKO TIVII AU SIO?
MHISHIMIWA NI HIVIII, NIMEMPANGIA HOTELI 'SHEMELA' ASIAMBUKIZE WATOTO UGONJWA WA MACHO NA HATA WEWE UKIRUDI USIYAPATE
KWA KUKUSHUKURU SIJUI NING'OKE NA MENO YAKO YA BARAZANI?!
HII 'RED EYES' ISHAKUWA FASHENI KILA MTU ANA-REMBUA KIVYAKE!
AFADHALI BABA UMEWAHI KABLA HUJAWA 'USIYEONA'
KUNA MTU ANA-TAKA AKUCHUKULIE MKEO ANAKUPOFUA ILI WAKITOKA NA MKEO USIWAONE
WE BABA WE! MBONA MKE NIMEZIKA KITAMBO SANA!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...NGUVU KAZINI, SIFA UKWENI

# Meli ya Uingereza yalipuliwa ikikatiza bahari ya shamu

**WASHINGTON,** MAREKANI

HALI inazidi kuwa tete katika eneo la Mashariki ya Kati baada ya juzi meli moja ya mafuta kuwaka moto kwenye bahari ya shamu baada ya kushambuliwa na wapiganaji wa Houthi.

Nahodha wa meli hiyo amesema meli yake ilishambuliwa kwa kombora usiku wa kuamkia Ijumaa na kusababisha mlipuko wa moto. Kundi la Houthi linatawala nchi ya Yemen na liliipiga meli hiyo inayoitwa Marlin Luanda kama njia ya kulipiza kisasi kwa mauaji yanayofanywa na Israel Ukanda wa Gaza.

Nahodha huyo aliiambia BBC kwamba mashambulizi hayo yalisababisha moto katika tangi moja la mizigo la meli hiyo na vifaa vya kuzima moto vilikuwa vikitumiwa kuuzuia.

Jeshi la Marekani lilitoa taarifa kuwa tukio hilo limesababishwa na wapiganaji wa Wahouthi baada ya kuipiga meli hiyo kwa kombora la balestiki.

Kamanda Mkuu wa Marekani alisema hadi jana hakuna majeruhi aliyeripotiwa.

Shambulio hilo limefanyika muda mchache dhidi ya meli za kibiashara, huku Wahouthi wanaoungwa mkono na Iran wameapa kuendeleza mashambulizi katika Bahari ya shamu.

Kundi hilo lilisema kuwa wanalenga meli zote zinazopita katika eneo hilo kwa ajili ya kuwaunga mkono Wapalestina wa Gaza, ambako wanakabiliwa na mapigano makali yanayofanywa na Israel.

Nchi za Marekani na Uingereza zimeanzisha mashambulizi ya angani dhidi ya wahouthi kujibu mashambulizi hayo, lakini bado wapiganaji hao wanaonyesha wana nguvu.

Msemaji wa Houthi alidai kuwa Marlin Luanda ilikuwa meli ya Uingereza na ililengwa kulipiza kisasi kutokana na uchokozi wa Marekani na Uingereza dhidi ya nchi yao.


Meli hiyo ya mafuta inapeperusha bendera ya Visiwa vya Marshall na inaendeshwa na kampuni ya Trafigura mtandao katika nchi 50 duniani, ikiwamo na Uingereza.

Serikali ya Uingereza ililaani mashambulizi dhidi ya meli za kibiashara na kueleza hayakubaliki. Wakati huo huo, wanajeshi wa Marekani wamesema waliharibu kombora la masafa marefu lililokuwa tayari kufyatuliwa na waasi wa Houthi wa nchini Yemen kuzilenga meli zinazopita kwenye Bahari ya Shamu.

Kamandi Kuu ya Marekani eneo la Mashariki ya Kati ilisema hayo jana kupitia mtandao wa X.

Ilisema iliainisha kombora hilo lililokuwa katika eneo linalodhibitiwa na wanamgambo hao, lilikuwa kitisho dhidi ya meli zake za kivita na za kibiashara zinazopita kwenye njia hiyo ambayo ni muhimu ulimwenguni.

**BBC**



Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, Annalena Baerbock akizungumza na Rais wa Sudan Kusini Salva Kiir wakati akiendelea na ziara yake barani Afrika jana. **PICHA:DPA**

# Marekani yaidhinisha uuzaji ndege vita kwa Uturuki

**WASHINGTON,** MAREKANI

SERIKALI ya Marekani imeidhinisha uuzaji wa ndege mpya za kivita 40 aina ya F-16 kwa nchi ya Uturuki zenye gharama ya dola bilioni 23.

Uuzaji huo ulicheleweshwa kwa muda mrefu baada ya Uturuki kuridhia nchi ya Uswizi kujiunga na Jumuyia ya Kujilinda ya Nchi za Ulaya (Nato).

Mpango huo unajumuisha pia vifaa 79 vya kisasa.

Uturuki iliidhinisha kujiunga na Nato ya Uswizi baada ya kuchelewa kwa zaidi ya mwaka mmoja na kusababisha mvutano ndani ya muungano huo.

Nchi hiyo ilituma ombi la ndege hizo kwa mara ya kwanza mwaka wa 2021, lakini kuchelewa kwake kuridhia kukubaliana na Uswisi kulionekana kuwa kikwazo kwake.

Uturuki ilikuwa na wasiwasi juu ya nchi hiyo kudaiwa kuunga mkono viongozi wa Wakurdi wanaotaka kujitenga.

Wabunge wa Uturuki waliridhia ombi la Uswizi wiki hii na Rais wa nchi hiyo Tayyip Erdogan alitia saini ya mwisho.

Rais wa Marekani Joe Biden, aliamrisha mauzo ya ndege hizo za F-16 yaidhinishwe bila kuchelewa.

"Kuidhinishwa kwangu kwa ombi la Uturuki la kununua ndege za F-16 kumetokana Uturuki kuruhusu uanachama wa Nato kwa Uswizi," alisema Seneta wa Democratic Ben Cardin, ambaye ni mwenyekiti wa Kamati ya Seneti ya Mahusiano ya Kigeni.

Alisema rekodi ya haki za binadamu kwa Uturuki inahitaji kuboreshwa, pamoja na kuiwajibisha Russia kutokana na uvamizi wake kwa Ukraine.

**BBC**

# Burkina Faso yapata chakula kutoka Russia

**OUAGADOUGOU,** BURKINA FASO

BURKINA Faso imepokea tani 25,000 za ngano zilizotolewa na Russia kama sehemu ya msaada wa tani 200,000 zilizoahidiwa na Rais Vladimir Putin kwa nchi kadhaa za Afrika.

Rais Putin wakati wa mkutano na viongozi wa Afrika katika mji wa Saint Petersburg Julai 2023, alitoa ahadi ya kusambaza nafaka bila malipo kwa nchi sita za Kiafrika, ikiwa ni pamoja na Burkina Faso. Nchi nyingine zinazonufaika na msaada huo ni Mali, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Eritrea, Zimbabwe na Somalia.

Waziri wa Mshikamano na Hatua za Kibinadamu, Nandy Somé Diallo, alihudhuria hafla ya makabidhiano iliyofanyika mji mkuu wa Ouagadougou.

"Serikali ya Burkina Faso imefurahishwa na zawadi muhimu katika kuwahudumia watu walioikimbia makazi yao kutokana na vurugu za wanamgambo na watu walio katika mazingira magumu," alisema Diallo.

# Serikali ya Kenya yaipinga mahakama

**NAIROBI,** KENYA

SERIKALI ya Kenya imeapa kupinga uamuzi wa mahakama dhidi ya hatua yake ya kutaka kupeleka kikosi cha polisi nchini Haiti.

Kikosi hicho kitaongoza ujumbe wa kulinda amani nchini humo ili raia kudumisha sheria na utaratibu unaoungwa mkono na Umoja wa Mataifa.

Jaji wa Mahakama ya Juu nchini Kenya Enock Chacha Mwita, alitoa uamuzi wa mahakama hiyo juzi akisema uamuzi wowote wa chombo chochote cha serikali ama ofisa wa serikali wa kupeleka kikosi cha polisi nchini Haiti unakiuka katiba na sheria, hivyo basi ni kinyume cha sheria.

Baada ya maamuzi hayo, msemaji wa serikali Isaac Mwaura, alijibu tamko hilo la mahakama kwa kueleza kuwa wakati serikali inaheshimu utawala wa sheria, imechukua hatua ya kupinga uamuzi wa mahakama hiyo mara moja.

Mwaura aliongeza kuwa serikali inasisitiza kujitolea kwake katika kuheshimu majukumu ya kimataifa.

Hata hivyo, Ekuru Aukot, ambaye ni mwanasiasa wa upinzani aliyepeleka ombi la kupinga kupeleka polisi nchini Haiti, alisema yuko tayari kwa mapambano ya muda mrefu.

**DW**

SAFU

MAKALA

# SABABU ZA MABADILIKO YA TABIA KWA WANAFUNZI WA VYUO VIKUU



Na Magabilo Masambu

**Kwa hiyo, iwapo mwanafunzi hatatambua kuwa ametumwa na taifa lake kuja kupata elimu kwa manufaa ya taifa, vilevile ikiwa mwanafunzi atasahau umasikini uliyomo katika familia yake na kujifananisha na wale anaowakuta vyuo vikuu wenye maisha mazuri, akawa na tamaa ya kumiliki vitu ambavyo wazazi wake hawana uwezo kumnunulia, lakini zaidi akakosa washauri wazuri wa namna ya kuendana na maisha ya chuo kikuu, basi uwezekano wa mwanafunzi huyo kuharibikiwa utakuwa mkubwa sana.**

VYUO vikuu vinachukuliwa kama sehemu muhimu sana kwenye maisha ya wanafunzi katika kujenga kesho yao. Mwanafunzi anayefika chuo kikuu, anachukuliwa kama mtu mzima, hivyo taratibu zilizokuwa zikitumika katika malezi kwenye taasisi za chini kama sekondari hazitumiki zikiwa ni pamoja na kuwabana kwa kanuni na sheria za shule.

Vilevile sheria zilizokuwa zikiwabana wawapo majumbani nazo sasa hulegezwa kwa kuamini kwamba wamekuwa watu wazima.

Lakini kwa baadhi ya wanafunzi hali ni tofauti. Wako wanaotambua kuwa kwa kufika kwao vyuo vikuu, sasa wamekuwa watu wazima ambao hawahitaji kusimamiwa. Lakini wako ambao wanafikiri kusimamiwa na kwamba kama hakuna taratibu za kuwasimamia wanaona sasa ndiyo nafasi pekee ya kufanya yale ambayo hawakufanya walipokuwa katika shule za sekondari, kama vile uvutaji wa sigara, ulevi na kadhalika.

Wako ambao wamekuja na tabia zao kutoka huko na wapo ambao hujifunza wakiwa vyuoni. Sababu za kujifunza zaweza kuwa ni pamoja na kutotambua hasa nini kimewaleta, ushamba na ulimbukeni wa kujifunza mambo kutokana na makundi, kukosa malengo makubwa katika maisha, kujiona kama bado wangali watoto wadogo, kutamani maisha wasiyokuwa nayo hata walikotoka, kujilinganisha kimaisha na baadhi ya rafiki zao. Zaidi ni kutotambua hali za maisha katika familia walimotoka.

Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere amewahi kusema kijana anayepata au aliyepata elimu ya chuo kikuu, anafananishwa na kijana anayeishi katika kijiji chenye njaa ya chakula. Wanakijiji wanampatia chakula kidogo kilichobaki ale ashibe, ili apate nguvu ya kwenda kijiji cha jirani kutafuta chakula kwaajili ya wanakijiji na kwamba ikiwa kijana huyo atakwenda kutafuta chakula alikotumwa akakipata na asikilete kijijini kwao penye njaa na taabu, basi kijana huyo atakuwa ni msaliti.

Wale ambao ni wapenzi wa sinema, mtaikumbuka sinema ya "Home Back" kijana alivyopambana kurudisha kichwa cha mungu wao, baada ya kuibiwa kijijini kwao hali iliyosababisha ukame, vifo vilivyotokana na njaa.

Ndivyo ilivyo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu kwamba wanapokuja vyuoni, wazazi jamii na taifa kwa ujumla wametumia chakula kidogo walicho nacho, kuwafanya wawe na nguvu ya kufika vyuo vikuu, matarajio yao ni kuona watoto wakirudi kuja kupambana na umasikini uliyoko kwenye taifa, jamii na familia kwa ujumla. Sasa, ikitokea ama wakapata elimu na isiwasaidie au wakashindwa kuipata kwa tabia zao kubadilika, hao watachukuliwa kama wasaliti.

Maneno ya Mwl.Nyerere yalikusudia kuwapa moyo na kuonyesha umuhimu wa wanafunzi wa vyuo vikuu katika taifa, jamii na familia kwa ujumla.

Kwahiyo, wanafunzi walipokuwa wakijiunga na elimu ya juu fikra ya kwanza walitambua wanalodeni kwa taifa hata kabla ya famlia zao na ndiyo maana tunaweza kuona tofauti ya wasomi wa zamani na sasa katika suala zima la uadilifu wa mali za umma.

Sasa hivi wasomi wengi mtazamo wao mkubwa ni juu ya familia zao zaidi kuliko nchi kwanza, wako wanaosema pengine gharama kubwa zinazotumika kuipata elimu bora pamoja na mikopo ya vyuo vikuu imeleta tabu kidogo, kwamba wanaona kama wanajisomesha hawasomeshwi na nchi, kwa sababu pesa wanazopewa watakuja kuzirudisha na kwamba zamani watu walisomeshwa bure.

Kwa hiyo ndiyo maana walifikiria zaidi taifa kabla ya familia zao lakini sina hakika kama hii inaweza kuwa sababu ya ubadhirifu wa fedha za umma!

Kwa hiyo, iwapo mwanafunzi hatatambua kuwa ametumwa na taifa lake kuja kupata elimu kwa manufaa ya taifa, vilevile ikiwa mwanafunzi atasahau umasikini uliyomo katika familia yake na kujifananisha na wale anaowakuta vyuo vikuu wenye maisha mazuri, akawa na tamaa ya kumiliki vitu ambavyo wazazi wake hawana uwezo kumnunulia, lakini zaidi akakosa washauri wazuri wa namna ya kuendana na maisha ya chuo kikuu, basi uwezekano wa mwanafunzi huyo kuharibikiwa utakuwa mkubwa sana.

Ushauri wangu, kila mwanafunzi aliyeko chuo kikuu lazima awe na malengo makubwa kwenye maisha ili kuwa kama kinga yake dhidi ya kujiingiza katika matendo machafu, kila atakapotaka kutenda anafikiria mimi muda si mrefu nitakuwa kiongozi wa nchi hii, pili kila wakati jaribu kufikiria maisha ya nyumbani kwenu na kwamba wewe ndiye mkombozi wa hali hiyo, tatu kila unachokitaka leo uwe na matumaini kuwa utakipata kesho ukiwa na kazi ambayo imetokana na elimu yako, kwahiyo ni suala la muda tu.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es Salaam-Tanzania**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Ndugu wagawana mali za marehemu, wamtimua mjane na watoto wake*



Na Adam Fungamwango

ULIKUWA ni msiba mzito kwa mwanamama huyo kwani mumewe alifariki na kumuachia watoto wadogo wawili.

Wakati akiwa na simanzi ataishi vipi, ndugu wa marehemu walikuwa kwenye kampeni kabambe ya kugawana mali.

Wakakusanya kila kilichokuwa kwenye nyumba ya ndugu yao, wakakitia kwenye lori na moja kwa moja safari ikaanza kwenda kuzika kijijini.

Hawakumjali hata mke wa marehemu na watoto wake. Wakamwambia tu pale tena hana chake kwa sababu aliyekuwa anamuweka ameondoka, hivyo afanye utaratibu mwingine wa maisha na watoto wake.

Ndugu wakachukua kila kitu pamoja na mwili wa ndugu yao kuelekea kijijini, mke yeye akaambiwa arudi kwao, ina maana asilione hata kaburi la mumewe.

Ni tukio la kweli lililotokea mwanzoni mwa miaka ya 1980 maeneo ya Magomeni jijini Dar es Salaam.

Mwanamuziki Cosmas Thobias Chidumule alikuwa anapita maeneo hayo akiwa anakwenda kwa rafiki yake maeneo ya jirani hapo akakutana na tukio hilo.

Akamkuta mke wa marehemu analia na mambo matatu. Kwanza kufiwa na mumewe, mtu wake wa karibu, anayempenda, ambaye muda wote wapo naye, kwa shida na raha.

Pili kaachiwa watoto hajui atawatunza vipi huku ndugu wa marehemu wakiwa wamezuia mali zote kwa lengo ya kugawana wenyewe msiba utakapoisha.

Tatu ni kwamba hatoona mtu aliyempenda kwa dhati anazikwa vipi na huenda hata kaburi lake asilione milele. Hili lilimliza sana.

Chidumule aliyekuwa mwanamuziki wa bendi ya DDC Mlimani Park wakati huo aliliona tukio lile na hata alipofika kwa rafiki yake ambaye alikuwa hakai mbali na msiba ulipotokea alimsimulia kile alichokiona. Wakasikitika wote, maisha yakaendelea.

Kwa mwanamuziki au msanii tukio lile halikupita hivi hivi. Hakupata usingizi mpaka akalitungia wimbo.

Akauita 'Mnanionyesha Njia ya Kwetu.' Ukarekodiwa kwenye studio za Redio Tanzania Dar es Salaam, mwanzoni mwa miaka ya 1980 na kupata umaarufu mkubwa.

Ni kwa sababu kipindi hicho bado wanawake wengi walikuwa hawajajua haki zao, wakadhulumiwa mali za waume zao na kuachwa wajane na mafukara.

Ingawa mpaka sasa jamii za Kiafrika bado zina tabia hii, angalau kwa sasa elimu kwenye televisheni, mitandao ya kijamii, magazeti na redio, imepenya na kinamama wengi kiasi kwamba wamekuwa wakizipata haki zao kupitia wanasheria, asasi za kijamii na hata mahakamani.

Labda tu aache mwenyewe kwa kuogopa mambo mengine lakini kwa sasa wanawake wakiamua 'kukomaa' hawadhulumiwi tena. Wimbo wa Chidumule ambaye kwa sasa ni mchungaji na anaimba nyimbo za Injili.

"Mnanionyesha njia ya kwetu, huku mnanisimanga kuwa sina changu tena, wala faida kwenu.

Hata tanga bado halijaisha ha, mnaanza kugawana mali ya marehemu mume wangu hehehe.

Ninapouliza yamekuwaje, jibu ni kwamba mnagawana mali ya mwanenu.

Mbona mmesahau, ya kuwa mali hiyo haswa, ni ya watoto na msimamizi ni mimi mama yao, ambaye leo mnanikana."

"Kama ni mila tuache, oooo hoo tuache kwa sababu madhara yake ni makubwa.

Mlikuwa mkiniita mke ooo, wengine shemeji, wengine wifi ooo, lakini yote mmeyasahau, kama ni msiba ni wa kwetu sote, kama ni msiba mama ni wa kwetu sote."

"Madhara yake ni makubwa ooo, madhara yake ni makubwa, madhara yake ni makubwa ooo, madhara yake ni makubwa.

Wengine mliita shemeji oooo, madhara yake ni makubwa, wengine mliita mimi wifi ooo, madhara yake ni makubwa, wengine mliita shangazi ooo.

Madhara yake ni makubwa hoo hoo hoo, madhara yake ni makubwa.

Wengine mliita shemeji oooo, madhara yake ni makubwa, wengine mliita mimi wifi ooo, madhara yake ni makubwa, wengine mliita shangazi ooo."

Kwa mujibu wake mwenyewe Chidumule siku moja akiimba wimbo huo kwenye ukumbi wa DDC Kariakoo, alipanda mwanamke mmoja na kumfuata, akamkumbatia kwa furaha, akaanguka chini na kuzirai.

Baada ya kupatiwa huduma ya kwanza, akajitambulisha kuwa yeye ndiye yule mwanamke aliyedhulumiwa mali, na baada ya wimbo huo kutoka redioni aliambiwa na rafiki yake Chidumule aliyemtembelea siku ile alipokuta tukio kuwa wimbo huo ulitungwa kutokana na tukio lake kwani wakati anakuja kumtembelea siku ile aliliona tukio na akalitungia wimbo.

Mwanamke huyo akasema ndiyo maana ameitafuta bendi iliyopiga wimbo huo na mtunzi amempata.

Kuzirai kwake ilikuwa ni hisia zilizopitiliza kumuona kwa mara ya kwanza mtunzi wa tukio lake, pia kuvuta kumbukumbu ya yale waliyompata huko nyuma, kwa sasa ni mjasiriamali na mambo yake si mabaya sana, maisha yanaendelea.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

SAUDA, binti mmoja mrembo anapata mwanaume na kubahatika kuolewa, lakini anakwenda kuishi kwenye nyumba ya familia ambayo mumewe Kassim na dada yake Havijawa wameirithi kutoka kwa baba yao mzazi. Binti aliona anakwenda kuishi kwa amani ili atengeneze familia yake, lakini kinachomkuta huko anajuta hata kwa nini alikubali kuolewa. Mara nyingi kuolewa ni jambo la kheri, lakini kwa Sauda inakuwa kinyume chake, kwani anakutana na wifi mtata, mkorofi, mmbea, mchonganishi ambaye anaiweka ndoa ya binti huyo aliyeolewa na kaka yake kuwa ya mashaka, tabu, huzuni, isiyokuwa na amani.Hali hii inamchosha Sauda na kulazimika kudai talaka kurudi kwao? Fuatilia kisa na mkasa huu unaosimuliwa kwenye gazeti hili la Nipashe pekee.

## Wifi Kichefuchefu-8

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

SAUDA aliangua kicheko na kusahau kama muda mfupi tu uliopita alikuwa akilia.

Akakumbuka jinsi Kassim alipokuwa akipita eneo lile, ambapo baada ya kuwazoa akaanza kuwatania, huku yeye ndiye akitaniwa zaidi kutokana na kila alipokuwa akipita alikuwa amepakatia mdoli.

Alikumbuka mbali jinsi alivyolazwa hospitali na Kassim alikwenda kumtazama siku za awali kabisa, kabla hata hawajaingia kwenye ulimwengu wa mapenzi.

Akakumbuka jinsi alivyolipia nusu ya matibabu yake, na Paulina pamoja na Pili walivyomwita jina la Baba Matokeo baada ya kukipita kitanda alichokuwa amelazwa.

Kwa wakati huo hata jina lake walikuwa hawalijui, bali ule tu utani wake wa kutoa jina hilo kwa mdoli wa Sauda, uliosababisha, Kassim kuitwa baba Matokeo, na Sauda naye kuwa mama Matokeo. Utani uliogeuka ukweli na kuanza kuwa wapenzi, baadaye ndoa.

"Basi Paulina sitokubali tena, nitapambana." Sauda akasema kionekana amefarijika.

********************************

"Hivi mume wangu, mimi nimeolewa na watu wangapi humu ndani?" "Kwa nini unasema hivyo mke wangu?

"Nasema hivyo kwa sababu hakuna hata siku moja wewe umewahi kuniamrisha niamke asubuhi asubuhi nikafanye usafi. Mimi mwenyewe hajua wajibu wangu, sasa kwa nini dada yako anakuja kunipigia kelele asubuhi hapa?"

"Havijawa huyo?"

"Sasa una dada gani mwingine?"

"Lini hiyo?"

"Jana, wewe uliondoka alfajiri hapa!" "Kaja kanifurusha hapa, tena inaonekana alijua wewe umeondoka! Halafu sasa siyo kama sikuwa nimefanya usafi. Ulipoondoka nilikwenda kufanya usafi, varandani, bafuni, chooni na uwanjani, lakini kote akaenda tena kuchafua kote, kaenda kuokota majani niliyotupa jalalani kayaridishia tena uwanjani, halafu anakuja kuniita tena eti niamke nifanye usafi! Unajua yule dada yako kanitibua, hawezi kunifanyisha kazi mara mbilimbili yule, nimemsitahi kwa pua tu."

"He, kumbe ndiyo imefikia huku mke wangu?"

"Habari ndiyo hivyo, ila niachie mimi mwenyewe. Wewe




**"Usimuogope Sauda, sisemi kama umpige, au mpigane, lakini usiwe mnyonge, akikubwatukia na yeye mbwatukie, atakuogopa. Usimuendekeze. Hutoona raha ya ndoa na ipo siku utaamua tu kufungasha virago urudi nyumbani."**

usimuulize!"

"Kwa nini?"

"Kalianza mwenyewe, mimi nitalimaliza, kama kakaanga mbuyu, basi wenye meno tupo tutatafuna."

"Sasa mbona unanitisha mke wangu, unataka kumfanya nini?"

"Wala, usiwe na wasiwasi, simfanyi chochote kile. Unajua dada yako anaona mimi niko kimya ananiona mshamba sana. Mimi si ulionea hapa hapa, mtaa wa pili kule! Ulinionea Kondoa wewe? Kule si ulikuja kunioa tu? Sasa kama hajui kuwa mimi mtoto wa Dar, atanijua!"

Maneno hayo yalimpa shida kidogo Kassim. Alijua dada yake Havijawa ni mkorofi, lakini hakujua mkewe Sauda anachotaka kukifanya.

************************************

"Mtoto si nguo utaomba mtu, ukikosa wako eee utalia sana mama. Wenzangu wana watoto mimi sina hata wa dawa, kila nikimuona mtoto wa mwenzangu uchungu nitabaini, niwatumapo wana na wenzangu mama zao hunisimanga..." Havijawa alikuwa anaimba wakati akifagia. Siku hiyo ilikuwa zamu yake ya kufanya usafi. Ilikuwa ni wiki moja baada ya tukio la kumchafuliwa mwenzake sehemu alizofanya usafi.

Aliimba wimbo wa zamani sana wa George Mukabi, akachanganya na wa Dk Remmy Ongalla.

Zote zilikuwa na maudhui yanayofanana. Ni ya mtu anayelilia mtoto. Sauda wala hakutaka kujisumbua kuumiza kichwa kuwa anaimbwa yeye, kwa sababu ndoa ilikuwa imetimiza miezi tisa sasa bila dalili zote za ujauzito.

Pamoja na kwamba ilikuwa mapema sana kwake na mumewe Kassim, lakini ilikuwa nongwa kwa wifi yake Havijawa.

Sauda akamsogelea karibu na pale alipokuwa akifagia, akamuuliza,"hivi wifi unanitafuta nini hasa? Nilichokulia wewe niambie ili nikurudishie, maana kila siku maneno maneno humu ndani!"

"Kipi ninachokutafutia?" Akauliza Havijawa. "Naona kila siku unanitafutia visa. Kila siku unanichokonoachokonoa, sijuelewi ujue!"

"Hivi nikuchokonoe kwa kipi haswa?"

"Mara usafi, mara nakula sana, mara sijui kutembea, mara nanepeana, mara mpaka sasa sina ujauzito, wewe inakuhusu nini lakini?" "Mimi si nimeimba tu hapa wimbo! Nimekutaja wewe kuwa huna ujauzito?" "Fumbo mfumbie mjinga bibi wewe, mwerevu anang'amua kwa haya yote unayonifanyia humu ndani, basi hata hili nalo unanifanyia mimi. Wimbo huu unaniimbia mimi. Hivi wewe uko sahihi kuulizwa swali hili? Wa kuniuliza hilo swali si yupo?" "Nani?"

"Kaka yako, yeye ndiyo anaweza kuniuliza hilo swali kwa sababu ndiyo aliyenioa, siyo wewe!" Sauda aliongea kwa hasira.

Kwa jinsi alivyosimama karibu na wifi yake, hasira ilivyompanda, Havijawa alihisi hatari ya kuvamiwa muda wowote ule, akaacha kufagia na kusogea nyuma taratibu, halafu alipofika mbali kidogo akageuka na kumwambia, "hunijui eee, sasa ndiyo utanifahamu kama mimi ndiyo Havijawa au nani!" Akamtishia.

************************************

"Mume wangu kuna jambo linaniumiza moyo!"

"Umeshaanza, yaani humu ndani nikisikia hivyo tu najua tayari kimeshanuka na Havijawa."

"Kama ulikuwepo!"

"Nini tena safari hii?"

"Mtoto."

"Mtoto gani?"

"Anataka mtoto."

"Kwani sisi tumemkataza kuwa na mtoto?"

"Anataka wa kwangu. Yaani mimi niwe na mtoto."

"Unajua wewe na huyo Havijawa mnanichanganya."

"Mume wangu Kassim, wewe mwenye unajua kuwa tangu dada yako aachwe na bwana 'ake arudi hapa amani hakuna. Sema mimi ni mvumilivu tu."

"Kwa hiyo mmegombana naye nini tena? Ndiyo huyo mtoto?"

"Anasema sijui anauliza kuwa haoni mimba, mtoto, wala dalili." Maneno hayo yalimfanya Kassim atikise kichwa na kutoa kicheko ambacho si halisi.

"Hivi dada yako anaweza kuniuliza maswali kama hayo? Yanamhusu nini? Swali hili ilibidi uniuze wewe kama mume wangu."

"Ni kweli, hujakosea kumjibu hivyo! Uko sahihi, mimi ndiyo mumeo niliyekupenda nikakuoa, kwa hiyo usimsikilize mtu yoyote zaidi ya mimi tu mumeo. Mpumbavu dawa yake ukae kimya tu."

"Sawa mume wangu, lakini nakuomba kaa ongea na Havijawa, asinichanganye, nikamchanganya. Masuala ya kunifuatilia mimi siyataki, yeye siyo mama mkwe wangu. Sijabahatika kumkuta mama mkwe wangu, ameshafariki, yeye nani? Kuna siku utakuja kuta ndani utakuta nishamvuruga dada yako na mimi nisharudi kwetu. Siyo kwa kukimbia ndoa, ila kuogopa mkono wa sheria!"

"Ina maana unampiga?"

"Yeye mwenyewe keshanitishia maisha eti nitamfahamu kama yeye ndiyo Havijawa au nani. Ana maana gani?"

Maneno ya mkewe na ambayo ameambiwa ameyasema dada yake yalimtisha zaidi Kassim kuliko hata matendo yenyewe. Akaona wanapokwenda mkewe Sauda na dada yake Havijawa si kuzuri.

INAENDELEA JUMAPILI




# 'UNABAKI KUWA MUNGU' YAMPAISHA DK SAM MAHENE

SIKU chache baada ya kuachia wimbo wake mpya, 'Unabaki kuwa Mungu', mwimbaji wa Injili nchini, Daktari Samwel Mahene, amewashukuru wapenzi wa muziki huo kwa mapokezi mazuri.

Akizungumza na Nipashe, Dk Mahene ambaye mbali na sanaa ni daktari wa binadamu, amesema wapenzi wa muziki huo wamemuonyesha upendo wa kipekee katika huduma yake na kumuunga mkono kupitia wimbo huo aliomshirikisha Godfrey Steven.

"Kuanzia kwa wapenzi wa muziki wa Injili hadi wadau mbalimbali wamenipokea vizuri kupitia wimbo huu Unabaki Kuwa Mungu, kwani umewapatia baraka kwa wengi na kugusa maisha yao ya kawaida na kiroho. Wimbo umebeba ushuhuda wa maisha ya watu ndio maana umeweza kupata mafanikio haya," amesema Dk Sam Mahene.

# Nyota ndogo aonya atamroga mume wake akichepuka



MWANAMUZIKI mkongwe nchini Kenya, Mwanaisha Abdalla, maarufu kama Nyota Ndogo, amemuonya mume wake ambaye ni mzungu anaweza kumroga endapo atamuona hatulii kwenye ndoa.

Akiandika ujumbe katika ukurasa wake wa Instagram, katika kumtakia heri mume wake ambaye alikuwa akisherehekea siku yake ya kuzaliwa, amesema mume wake huyo anampenda na kamwe hatatoa nafasi ya kumpoteza.

"Mume wangu nakupenda sana, labda uniache wewe lakini mimi siwezi kukubali kukupoteza. Ukileta ujinga nakuroga unarudi kwa laini," ameandika.

Alimsifia mume wake huyo mzaliwa wa Denmark kwamba ni ubavu wake wa pili na pia ni chaguo kutoka kwa Mungu, hivyo atahakikisha anamlinda kila siku ndani ya maisha yao.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SPURS YAPANDA DAU

TOTTENHAM Hotspur inaandaa dau la dakika za mwisho la pauni milioni 80 ili kumnunua kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Conor Gallagher, mwenye umri wa miaka 23, kutoka Chelsea. (***Football Insider***)

### HALL ATAKIWA BRIGHTON

KLABU ya Brighton ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili kiungo wa kati wa England, Kiernan Dewsbury-Hall, mwenye umri wa miaka 25 kutoka Leicester. (***Sky Sports***)

### OSIMHEN ANUKIA UNITED

KAULI ya Rais wa Napoli, Aurelio de Laurentiis, kuwa mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 25, ataondoka katika klabu hiyo msimu huu inaweza kufungua njia ya kuhamia Manchester United. (***Manchesyer evening News***)

### NAPOLI YAMKATAA MOURINHO

KOCHA wa zamani wa AS Roma, Jose Mourinho, mwenye umri wa miaka 61, hatakuwa kocha ajaye wa Napoli licha ya kuhusishwa na kazi hiyo. (***Marca***)

### VIEIRA ANUKIA MONACO

MONACO wameulizia Arsenal kuhusu mkataba wa mkopo wa kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ureno, Fabio Vieira, mwenye umri wa miaka 23. (***Football Transfers***)

### BOEY KUTUA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich imekubaliana na Galatasaray kumsajili beki wa kulia wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Sacha Boey, mwenye umri wa miaka 23. (***Fabrizio Romano***)

### COVENTRY: O'HARE HAUZWI

KLABU ya Coventry City inatazamiwa kukataa ofa yoyote kwa kiungo mshambuliaji wa England, Callum O'Hare, mwenye umri wa miaka 25, huku kukiwa na nia ya kumtaka kutoka kwa Burnley, Southampton na Leicester City. (***Football Insider***)

### CARSLEY AIKATAA IRELAND

KOCHA wa Timu ya Taifa ya England ya umri chini ya miaka 21, Lee Carsley, amekataa ofa ya kuinoa Jamhuri ya Ireland, ambayo aliichezea mechi 40 kwa matumaini ya kuibuka mgombea wa kiti cha Gareth Southgate kama kocha wa England. (***Mail***)

### ZIDANE AIGOMEA ALGERIA

KOCHA na mchezaji wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amekataa nafasi ya kuwa Kocha wa Timu ya Taifa ya Algeria. (***L'Equipe***)

### MRITHI WA KLOPP BADO

LIVERPOOL haina mrithi atakayechukua nafasi ya kocha Mjerumani, Jurgen Klopp, ambaye ataondoka Anfield msimu huu wa joto. (***Telegraph***)

### ALONSO KUTUA LIVERPOOL

KOCHA wa Bayer Leverkusen na kiungo wa zamani wa Liverpool, Xabi Alonso, Roberto de Zerbi wa Brighton na Ange Postecoglou wa Tottenham Hotspur ni miongoni mwa wanaowania kuchukua nafasi ya Jurgen Klopp. (***Times***)

### KLOPP AWAONDOA NYOTA

KUONDOKA kwa Jurgen Klopp kunaweza kushuhudia mlinzi wa Uholanzi, Virgil van Dijk, mwenye umri wa miaka 32, fowadi wa Misri, Mohamed Salah (31), na mlinzi wa England, Trent Alexander-Arnold (25), pia wakiondoka Liverpool. (***Sports***)

## DONDO A SOKA
## MAGAZET ULAYA



# KLOPP ATANGAZA KUONDOKA LIVERPOOL

## ●●● Aeleza hatarejea tena katika ngazi ya klabu...

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp ametangaza kuacha nafasi yake kama Kocha wa Liverpool mwishoni mwa msimu huu, akisema "imeishiwa nguvu."

Klopp mwenye umri wa miaka 56, ameleta mafanikio makubwa kwa Liverpool baada ya kuwasili Anfield mwaka 2015 na kuiwezesha klabu hiyo kunyakua taji la Ligi Kuu England mwaka, 2020 na Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019.

Lakini hii itakuwa kampeni yake ya mwisho kuinoa Liverpool, akitangaza ataondoka kwenye uwanja huo wa mwisho wa msimu huu.

Klopp atapumzika kutoka kwenye uongozi na akasema hatasimamia klabu au nchi kwa angalau mwaka mmoja. Pia alisema hana mpango wa kusimamia timu nyingine nchini England zaidi ya Liverpool.

"Ninaweza kuelewa ni mshtuko kwa watu wengi wakati huu, unaposikia kwa mara ya kwanza, lakini ni wazi naweza kuelezea, au angalau kujaribu kuelezea," alisema Klopp katika taarifa yake ya video iliyotolewa na Liverpool.

"Ninapenda kila kitu kuhusu klabu hii, napenda kila kitu kuhusu hili jiji, napenda kila kitu kuhusu mashabiki wetu, napenda timu, napenda wafanyakazi. Ninapenda kila kitu. Lakini kwa kuwa bado ninachukua uamuzi huu inakuonyesha nina hakika. ndiyo ninayopaswa kuchukua.

"Nipo, nitasemaje nikiishiwa nguvu. Sina shida sasa, ni wazi, nilijua tayari kwa muda mrefu itabidi nitangaze wakati mmoja, lakini niko sawa kabisa. Ninajua kuwa siwezi kufanya kazi hiyo tena na tena na tena na tena na tena."

Aliongeza: "Ukiniuliza sasa kama nitaisimamia tena timu nyingine, nitasema hapana. Lakini hujui ni wazi kwani sijawahi kuwa na hali hii. Lakini najua kwa hakika sitawahi kusimamia klabu tofauti na Liverpool nchini England, haiwezekano.

"Nitapata kitu kingine cha kufanya. Lakini sitasimamia klabu au nchi kwa angalau mwaka mmoja."

Katika taarifa hiyo ya hisia, Klopp alisema anawiwa na mashabiki wa Liverpool maelezo kwa nini anarudi nyuma sasa. Alisema ulikuwa uamuzi mgumu lakini pia alihisi "unafuu" alipoufanya, akisema ni wakati muafaka kwake kujaribu "maisha ya kawaida" na kuona ikiwa anakosa usimamizi.

"Itakuwa nzuri ikiwa unaweza kukubali uamuzi wangu kama mgumu, lakini sahihi," aliongeza Klopp. "Nahitaji kutafuta kusudi tofauti na kulitafuta."

"Niliiambia klabu tayari mnamo Novemba," alisema. "Lazima nielezee kidogo kwamba labda kazi ninayofanya watu wanaiona kutoka nje, niko kwenye simu na kwenye vikao vya mafunzo na mambo kama haya, lakini mambo mengi hutokea karibu na mambo ya aina hii, inamaanisha msimu unaanza na unapanga msimu ujao tayari.

"Tulipokaa pamoja tukizungumza juu ya uwezekano wa kusajiliwa, kambi ya majira ya joto ijayo na tunaweza kwenda popote, wazo likaja, 'Sina hakika kuwa niko hapa tena,' na nikajishangaa kwa hilo. Ni wazi nikaanza kufikiria kuhusu hilo.

"Haikuanza wakati huo, lakini kwa kweli msimu uliopita ulikuwa msimu mgumu sana na kulikuwa na wakati ambapo katika klabu nyingine pengine uamuzi ungekuwa, 'kwaheri, asante sana kwa kila kitu, lakini labda sisi inapaswa kugawanyika hapa, au kuishia hapa.' Hiyo haikutokea hapa.

"Kwangu mimi ilikuwa kubwa na kubwa, muhimu sana kwamba ningeweza kusaidia kurudisha timu hii kwenye reli. Ni nilikuwa nikifikiria tu. Nilipogundua mapema sana kwamba ilifanyika, ni timu nzuri sana na yenye uwezo mkubwa na yenye kundi la watu wa rika kubwa, wahusika wakuu na hayo yote, basi ningeweza kuanza kujifikiria tena na hayo yalikuwa matokeo. Siyo ninachotaka kufanya, ni kile ninachofikiri ni sawa kwa asilimia 100."

Klopp alijiunga na Liverpool Oktoba 2015 na kuwaongoza kurejea kwenye kilele cha soka la Uingereza na Ulaya. Chini ya Klopp, Liverpool walishinda taji lao la kwanza la ligi baada ya miaka 30 mwaka 2020, taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019, Kombe la FA mwaka 2022 na Kombe la Carabao mwaka 2022.

Pia aliwaongoza hadi fainali za Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2018 na 2022 na vilevile Fainali ya Ligi ya Europa mwaka wa 2016. Walishinda Kombe la UEFA Super mwaka wa 2019 na taji la Kombe la Klabu bingwa ya Dunia mwaka 2019.

Baada ya kampeni ngumu ya 2022-23, Klopp amesaidia kuirejesha Liverpool kileleni katika Ligi Kuu England msimu huu, kwa tofauti ya pointi tano dhidi ya Manchester City inayoshika nafasi ya pili baada ya mechi 21.

Liverpool bado wako kwenye mchanganyiko wa mashindano manne (Ligi Kuu, Kombe la FA, Kombe la Carabao na Ligi ya Europa) na Klopp atalenga tuzo katika kampeni yake ya mwisho Anfield.




# NAPOLI ILIJUA OSIMHEN ATAONDOKA

**NAPLES,** Italia

MMILIKI wa Napoli, Aurelio de Laurentiis amesema "nilijua" Victor Osimhen, huenda akaondoka mwishoni mwa msimu huu, na kuongeza anatarajia mshambuliaji huyo kujiunga na timu ya Ligi Kuu England, Real Madrid au Paris Saint-Germain.

De Laurentiis aliulizwa na vyombo vya habari vya Italia kutoa maoni yake baada ya Osimhen kudokeza juu ya kuondoka kwa majira ya joto kutoka Naples mapema wiki hii, akisema alikuwa ameamua juu ya mustakabali wake lakini atafichua tu mipango yake mwishoni mwa msimu.

"Tulijua hilo tangu msimu wa joto uliopita," alisema De Laurentiis akiwaambia waandishi wa habari.

"Ndio maana mazungumzo ya mkataba mpya yalikuwa yamekamilika na yalikuwa ya kirafiki... lakini tulijua kabisa angeenda Real Madrid, PSG au timu yoyote England."

Desemba mwaka jana, Osimhen mwenye umri wa miaka 25 alitia saini nyongeza ya mkataba na mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Italia, Serie A utakaomalizika Juni mwaka, 2026.

"Niko na Napoli, nilitia saini mkataba mpya. Ninafurahia muda wangu kule. Nafikiri tayari nimeshafanya maamuzi, tayari najua ninachotaka kufanya katika maisha yangu ya soka," alisema Osimhen akiiambia CBS Sports Jumanne.

"Tangu nimeanza, nimekuwa mtu wa kufanya maamuzi yangu mwenyewe na kila kitu kinakwenda sawa kwangu. Tayari najua hatua inayofuata ninayotaka kuchukua, hivyo kwa sasa nataka tu kumaliza msimu kwa nguvu."

Napoli iliripotiwa kukataa ofa ya zaidi ya euro milioni 200 kwa Osimhen kutoka timu ya Saudi Arabia msimu uliopita wa joto.

Mchezaji huyo bora wa Afrika alijiunga na Napoli kutoka Lille mwaka 2020 na kufunga mabao 26 katika kampeni ya 2022-23 na kuisaidia timu yake kushinda taji la Serie A.

Osimhen kwa sasa yuko kwenye Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), akiwa na Nigeria na jana Jumamosi walikuwa wakicheza dhidi ya Cameroon katika hatua ya 16 bora.

Laurentiis pia alikanusha Mourinho angechukua nafasi ya ukocha wa Napoli baada ya kutimuliwa kwa Walter Mazzarri.

Kufukuzwa kwa kocha huyo wa Ureno na AS Roma mapema mwezi huu kulizua tetesi nyingi kuhusu mustakabali wake na amekuwa akihusishwa na kuajiriwa Saudi Arabia na Napoli.

"Mourinho hana uhusiano wowote na Napoli. Ni kocha mcheshi na asiye na msukumo, lakini ninahisi hatima yake iko nje ya Italia. Hakika si Napoli," aliongeza.

## Misri watoa ng'ombe AFCON

**SAN PEDRO,** Ivory Coast

SHIRIKISHO la Soka la Misri (EFA), limetoa sadaka ya ng'ombe kwa nia ya kuipa timu hiyo bahati zaidi katika michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON).

Msemaji wa EFA, Mohamed Morad, aliliambia Shirika la Habari la Associated Press jana shirikisho hilo lilimchinja ng'ombe huyo na kusambaza nyama kwa watu wenye mahitaji jijini Cairo siku moja kabla ya mchezo wa leo dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Misri, ambayo bado haijashinda mchezo wowote, itacheza na DRC katika hatua ya 16 bora mjini San Pedro.

Safari ya timu kutoka Abidjan hadi San Pedro ilichelewa kwa saa moja Ijumaa.

Kampeni ya Misri imekumbwa na majeraha, huku wakimpoteza nyota na nahodha, Mohamed Salah kutokana na jeraha la msuli katika mchezo wao wa pili wa kundi, pia kipa, Mohamed El Shenawy, aliyeteguka bega katika mchezo wa mwisho wa hatua ya makundi.

Emam Ashour alilazwa hospitalini usiku wa kuamkia jana kwa matibabu ya mtikisiko baada ya kuumia kichwa akiwa mazoezini na tayari amejiunga tena na kikosi hicho.

Wachezaji wa Misri waliripotiwa kujitoa mhanga wakati wa mazoezi kabla ya kutwaa ubingwa wa Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka 2008 nchini Ghana.

Misri, ambao ni mabingwa mara saba, wametoka sare katika mechi zao tatu za makundi sawa na DRC.

# Guardiola: Sasa nitalala vizuri

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema "sasa nitalala vizuri zaidi " baada ya Jurgen Klopp kutangaza kuachana na Liverpool huku akidokeza anaweza kuongeza mkataba wake na Manchester City.

Klopp atajiuzulu mwishoni mwa msimu huu baada ya kushinda Ligi Kuu England, Ligi ya Mabingwa Ulaya, Kombe la FA, Kombe la Ligi, Super Cup na Kombe la Klabu Bingwa ya Dunia pale Anfield.

Liverpool walikuwa wamejiweka kama washindani wakuu wa Manchester City ya Guardiola wakati wa Mjerumani huyo pale England, na Guardiola alikiri atafurahi kuona mpinzani wake akiondoka.

"Nitalala vizuri zaidi," alisema, baada ya ushindi wa City wa bao 1-0 dhidi ya Tottenham Hotspur kwenye mchezo wa Kombe la FA uliochezwa juzi usiku.

"Siku moja kabla ya kucheza dhidi ya Liverpool ilikuwa karibu ndoto mbaya. Bila shaka atakosekana. Nilishtushwa, kama kila mtu, kwa habari. Nilihisi sehemu ya Manchester City ingepotea.

"Hatuwezi kufafanua kipindi chetu hapa pamoja bila yeye na Liverpool, haiwezekani. Wamekuwa wapinzani wetu wakubwa na binafsi amekuwa mpinzani wangu mkubwa tangu alipokuwa Borussia Dortmund na mimi nikiwa Bayern Munich.

"Nadhani Ligi Kuu itakosa haiba yake, haiba yake na jinsi timu zake zinavyocheza. Namtakia kila la heri."

Akizungumza juzi kufuatia taarifa iliyotolewa, Klopp alisema ameishiwa na nguvu zinazohitajika kuendelea kama Kocha wa Liverpool.

Hata hivyo, Guardiola alisema baada ya zaidi ya miaka saba kwenye Uwanja wa Etihad, bado hajakataa kuongeza mkataba wake unaotarajiwa kumalizika mwakani.

Alisema kwa shauku anaamini atakutana na Klopp tena kwenye mtandao, licha ya Klopp kusema kazi yake kama kocha inaweza kuwa imemalizika.

"Labda ni maoni ambayo hatakubali lakini atarejea," alisema Guardiola.

"Najua, labda katika muda wa miaka 10, anaweza kuhitaji kuongeza nguvu zake. Kwa utu wake na nguvu zake, atarejea. Timu ya Taifa, timu nyingine, sijui lakini soka linahitaji watu kama yeye.

"Sijambo. Nataka kuifanya bado kwa mwaka mmoja zaidi, na labda kuongeza. Niko sawa. Bado ninajaribu kusimamia."



## HABARI MICHEZO

### Safari ya Inonga, Simba yafunguka

INATOKA UK. 24

Aliongeza mkataba wa nyota huyo utamalizika mwakani na ikitokea ofa imewafikia, ndio suala la kumuuza au kuendelea naye litajadiliwa kwa kufuata mapendekezo ya benchi la ufundi linaloongozwa na Abdelhak Benchikha.

Wakati huo huo inaelezwa Benchikha ameitosa ofa ya kuifundisha Timu ya Taifa ya Algeria, ambayo imetimua kocha wake, Djamel Belmadi, baada ya kushindwa kufuzu hatua ya 16 bora ya fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON).

"Mimi ni Simba, nitaendelea kuwa Simba, nataka kushinda nikiwa na Simba, hili nilishalisema pia miezi sita iliyopita kuhusu mimi kujiunga na Timu ya Taifa ya Algeria haiwezekani, kwa sasa akili yangu ipo Simba na ninafuraha kuwapo hapa, nataka nishinde vikombe nikiwa na timu hii, na ninafuraha kuwa hapa, na nina furaha pia kuwa Tanzania na lazima niendelee na kazi yangu.

Ambacho wengi hawakijui mimi ni Kocha wa Simba, lakini mimi pia shabiki wa timu hii, na nina furaha na mashabiki wao, ninapambana kwa moyo wangu wote kwa ajili kushinda kila siku," Benchikha alisema.



# DK. MWINYI AAHIDI KUMALIZA UTATA Z'BAR UANACHAMA CAF

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar imesema iko katika mchakato wa kutafuta ufumbuzi kutokana na changamoto ya Timu ya Soka ya visiwa hivyo kukosa nafasi ya kushiriki katika mashindano mbalimbali ya kimataifa ikiwamo michuano ya Kombe la Mataifa Afrika (AFCON).

Kauli hiyo ilitolewa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wakati wa uzinduzi wa jezi za Timu za Taifa za Zanzibar uliofahyika hkwenye viwanja vya maonyesho Nyamanzi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja juzi.

Rais huyo alisema serikali inatambua changamoto iliyopo katika soka la Zanzibar hasa ushiriki wa timu za taifa katika mashindano ya kimataifa.

Alisema wanaendelea na jitihada za pamoja katika kutafutua ufumbuzi wa suala hilo na wanamatumaini makubwa jitihada hizo zitafanikiwa.

"Serikali inafahamu changamoto hii ya Zanzibar kutoshiriki mashindano makubwa kama vile AFCON na mengine ya kimataifa, hivyo tunaendelea na mchakato wa kulipatia ufumbuzi, naamini tutafanikiwa," alisema Mwinyi.

Aliongeza ameridhishwa na ubunifu wa jezi hizo na kusema zimetengenezwa katika viwango bora.

Alisema jezi hizo zitatumika katika mashindano makubwa ya kanda, kitaifa na kimataifa ambayo Zanzibar itapata nafasi ya kushiriki.

Aliongeza serikali itajenga viwanja katika kila wilaya ili kuongeza hamasa na uwezo wa Zanzibar kuandaa mashindano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa.

Naye Rais wa Yanga, Hersi Said, alilitaka Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), kuhakikisha mapato yanayopatikana kupitia jezi hizo yanaingia serikalini sio kwa mtu mmoja mmoja.

Hersi alisema mbunifu alitetengeneza jezi hizo ndiye aliyebuni jezi za Yanga ambazo zimekuwa zikiwaingizia Sh. bilioni 1.5 kila mwaka.

Mbunifu wa jezi hizo, Sheria Ngoi, alisema ametengeneza jezi hizo kwa kuweka vitu ambavyo vinapatikana Zanzibar.




Benson Mwakalinga, akiwa ameshikilia mfano wa hundi ya Sh. milioni 54.6 baada ya kushinda Multibet bonus ya asilimia 1000 kwenye kiasi chake cha ushindi kutoka SportPesa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mzize ajipanga 'kumteka' Gamondi

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Yanga, Clement Mzize, amesema hatakata tamaa na amejipanga kuendelea kujituma ili kumshawishi zaidi, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Miguel Gamondi, kumpatia nafasi ndani ya kikosi cha timu hiyo.

Mzize amesema hayo baada ya ujio wa mshambuliaji mpya, Joseph Guede, ambaye amechukuwa nafasi ya Hafiz Konkoni aliyetemwa katika dirisha dogo la usajili.

Nyota huyo aliyepandishwa kutoka timu ya vijana kwa sasa ni mmoja wa mastraika wanaotegemewa akishirikiana na kinara wa mabao ndani ya Yanga, Kennedy Musonda.

Alisema anatambua ushindani uliopo ndani ya timu hiyo hasa katika safu ya ushambuliaji, ataendelea kupambana na kujituma kwenye mazoezini na kila mechi atakayopewa kucheza anatarajia kuonyesha kiwango bora.

"Ni kweli katika nafasi ninayocheza kuna mtu ambaye amekuja kuleta ushindani ila kumbuka nyuma alikuwa Mayele (Fiston), lakini nilifanikiwa kucheza, ninaimani bado nitapata kwa sababu nitajituma, nitafuata maelekezo ya benchi la ufundi ili kupata nafasi ya kucheza," alisema Mzize.

Aliongeza wachezaji wa timu hiyo wamedhamiria kupambana kufanya vizuri katika kila mechi ili kuwapa furaha mashabiki wao na vile vile kutimiza malengo yao.

"Bado kuna nafasi ya kufanya vizuri, tunaamini ligi itakaporejea tutaendelea kuwapa furaha mashabiki, maandalizi ambayo tunayafanya yanatupa imani tutaimarika, mashabiki waendelee kuwa pamoja nasi," Mzize aliongeza.

# *Yanga: Azam 'wabaya wetu'*

INATOKA UK. 24

amfunge nani hapana," alisema kiongozi huyo.

Alisema anaamini kila mchezaji wa Yanga ana ndoto ya kufanya vizuri zaidi na kwa msingi huo, wamejiandaa kucheza katika kiwango bora kwenye kila mchezo ulioko mbele yao.

"Hatutadharau mechi, kwetu kila mechi itakuwa sawa na fainali, tunataka kumaliza hesabu mapema," Kamwe alitamba.

Yanga inajiandaa na mechi ya Kombe la FA dhidi ya Haulung FC kutoka Njombe ambayo bado haijapangwa itachezwa huku ratiba ya Ligi Kuu Bara ikionyesha itashuka dimbani tena Februari 16, mwaka huu kuwakabili 'Maafande' wa JKT Tanzania.

Baada ya hapo, itashuka kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Februari 23, mwaka huu kuwakaribisha CR Belouizdad katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika na itamaliza kibarua cha mechi za makundi Machi Mosi, mwaka huu ugenini Misri kuwafuata mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Al Ahly.

Yanga pia inashika nafasi ya pili katika msimamo wa kundi lao ikiwa pointi tano sawa na vinara Al Ahly, lakini ikiwa imezidi mechi moja zaidi na Waarabu hao ambao wameshuka dimbani mara nne.

Michezo
Jumapili Januari 28, 2024
Nipashe



Klopp atangaza kuondoka Liverpool

UKU. 21

# Yanga: Azam 'wabaya wetu'

## ●●● Yaota ufalme wa Bara huku ikitamba wakati wa kurejea...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha Yanga kikiendelea na mazoezi yake chini ya Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, mabosi wa timu hiyo wameweka wazi hawafurahishwi kuona Azam FC iko kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa muda mrefu.

Azam inaongoza ligi hiyo yenye timu 16 ikiwa na pointi 31 lakini imecheza mechi mbili zaidi huku Yanga inafuatia ikiwa na pointi 30 kibindoni.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, aliliambia Nipashe jana haijazoeleka kuona Azam inaongoza kwa muda mrefu, ikiwa kileleni kabla ya Desemba 23, mwaka jana wakati ligi hiyo iliposimama kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi na maandalizi ya Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON).

Kamwe alisema hali hiyo inawakwaza na wanafurahi kuona mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zitarejea hivi karibuni na wao, Yanga kurudi kwenye nafasi 'yao'.

"Ligi imesimama muda mrefu, Azam yupo juu ya msimamo tangu Desemba, kusema kweli wanatukwanza sana, maana jamaa watakuwa hapo hadi Februari, nina imani kama ingekuwa inaendelea saa hizi tungekuwa juu.

Ndiyo maana tumefurahi sana kurejea kwa ligi kwa sababu litakuwa ni suala la muda tu sisi kurudi kileleni, " alisema Kamwe.

Aliongeza Yanga imejipanga kuendelea kutoa 'dozi' katika kila mechi watakayocheza na hiyo ndio njia pekee ya kurejea kwenye 'hadhi' yao.

"Kwenye ligi yetu haijazoeleka yaani kukaa mwezi mmoja mpaka miwili, Yanga isikae kileleni, hii imetuuma na kutukwaza, lakini tunarudi, vijana wanajifua, nadhani ligi ikianza muda si mrefu tu tutakaa tulipopazoea," Kamwe alisema.

Alieleza hawana wasiwasi na mechi za Ligi Kuu pamoja na mashindano ya Kombe la FA, badala yake nguvu zao zaidi wanazielekeza kwenye michezo ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo wamebakiza mechi mbili dhidi ya CR Belouizdad ya Algeria na Al Ahly (Misri).

"Huku kwenye ligi na Kombe la FA wala hatuna shaka nako, ila Ligi ya Mabingwa tunaomba wanachama na mashabiki tushikamane kwa sababu mechi ni ngumu, tuna mechi hatari mbili za kimataifa, tukishinda tunakwenda moja kwa moja robo fainali, ambapo ndiyo lengo letu, lakini uzuri wake sio za kupiga ramli, sio nani

INAENDELEA UK. 23



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akicheza mpira katika sherehe maalumu za uzinduzi wa jezi mpya za Timu za Soka za Taifa za Visiwani humo. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

## Safari ya Inonga, Simba yafunguka

**Na Saada Akida**

WAKATI tetesi za kutakiwa kwa beki wa Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Henock Inonga, na AS FAR Rabat ya Morocco zikiendelea kusambaa, uongozi wa Simba umeweka wazi bado haujapokea rasmi ofa yoyote kuhusiana na mkongomani huyo, imeelezwa.

Kiwango cha Inonga kinadaiwa kumvutia aliyekuwa Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ambaye sasa anakinoa kikosi cha AS FAR Rabat.

Inonga bado yuko Ivory Coast katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika akiwa na DRC ambayo imetinga hatua ya 16 bora.

Thamani ya beki huyo wa Wekundu wa Msimbazi ambaye amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake ni Dola za Marekani 500,000.

Taarifa zilizopatika jijini Dar es Salaam zinasema kocha huyo amependekeza jina la Inonga kwa lengo la kukiongezea nguvu kikosi chake kinachoshiriki Ligi Kuu ya Morocco maarufu kama Botola League.

"Nabi amewaambia mabosi wa timu yake wanakikishe wanaipata saini ya beki wa Simba (Inonga), kwa ajili ya maboresho ya kikosi chake ingawa wanatambua hali halisi ya thamani ya mchezaji wenyewe ambaye bado ana mkataba unaotarajia kufikia ukingoni mwakani", kilisema chanzo chetu.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kwa sasa hawezi kuzungumza lolote kwa sababu bado hawajapokea ofa yoyote mezani kwao inayomhusisha beki huyo.

"Sisi kwa sasa hatuna jambo lolote la kusema, kama ni kweli au vipi kwa sababu uongozi bado hauna ofa yoyote inamhusisha Inonga na klabu yoyote zaidi tunaendelea na maandalizi ya ligi," alisema Ahmed.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >